# TAFSIRI YA
# TAJWEED – EL – QUR'AN TUKUFU


MTUNGAJI

**FAIZ ABDULQADIR SHEIKH AZZUR**

تأليف

**فائز عبد القادر شيخ الزور**

إجازة في اللغة العربية وآدابها

جامعة دمشق

إجازة في القراءات للقرآن الكريم

MFASIRI

**UMMU SALAH**

**SULTANATE OF OMAN**

# TAFSIRI YA
# TAJWEED – EL – QUR'AN TUKUFU

**MTUNGAJI**

**FAIZ ABDULQADIR SHEIKH AZZUR**

**تأليف**

**فائز عبد القادر شيخ الزور**

**إجازة في اللغة العربية وآدابها**

**جامع دمشق**

**إجازة في القراءات للقرآن الكريم**

**MFASIRI**

**UMMU SALAH**

**SULTANATE OF OMAN**

بسم الله الرحمن الرحيم

# DIBAJI

Sifa njema zote ni za Mwenyezi-Mungu, Mola wa viumbe vyote. Na sala na salamu zimshukie Mjumbe na Mtume wake wa mwisho Sayyidna Muhammad na Ali zake na Masahaba wake na waliowafuata kwa wema mpaka siku ya Malipo.

TunaMshukuru Mwenyezi-Mungu Mwingi wa Rehemu na Mwenye Kurehemu, kwa neema zaKe zisizohesabika wala zisizo mfano juu yetu kwa jumla, na hassa kwa kutuzindua na kutujaaliya kutafsiri kijitabu hiki ambacho tunaomba kiwe chenye faida kwa ndugu zetu.

Elimu ya Tajweed ni miongoni mwa elimu tukufu kabisa, kwa sababu ina alaqa kubwa na Kitabu Kitakatifu cha Mwenyezi-Mungu; na utajo wenye hekima kubwa. Kwa hivyo ni wajibu wetu sote kujifunza kuisoma vilivyo, kama Alivyomsomea Sayyidna Jibril (A.S), Mtume (S.A.W) na kama Mtume (S.A.W) Alivyowasomea Masahaba waKe na kama walivyoieneza jili baada jili mpaka ikatufikia sisi katika hali yenye kuhifadhika kabisa, na itabakia hivyo mpaka siku ya Qiyama kama ilivyosadikishwa kwa Qauli yake Taala: (إنا نحن نزّلنا الذّكر وإنّا له لحٰفظون) .

Nataraji na kuomba kwa Mola wetu Mtukufu Atupokelee amali zetu ijapo ndogo, na ziwe khaalisan liWaj’hihi-el-Karim.

Nawashukuru na kuwaombea Dua kutoka ndani ya moyo wangu walionishariki katika kazi hii kwa namna yo yote ile, Mola Awajaze kheri nyingi na ziwe katika mizani ya mema yao, Amin.

WasallaAllahu ala Annabiyyil-Rrahmah wa Imaamel-Muuminin wa AL hamdulillahi Rabil Alamin.

Ummu Salah

# FAHRASI

**Dibaji**

**Utangulizi**

**Darasa ya (1) Usomaji Bora wa Qur'an, na Njia za Usomaji............ 1**

**Darasa ya (2) Istiadha na Basmala.............................................. 4**

**Darasa ya (3) Lamu na Hamza Wasl............................................ 7**

**Darasa ya (4) Noon yenye Sukun na Tanween: Id'haar..................... 15**

**Darasa ya (5) Noon yenye Sukun na Tanween: Id'gham.................. 19**

**Darasa ya (6) Noon yenye Sukun na Tanween: Iqlaab na Ikh'faa...... 23**

**Darasa ya (7) Hukumu za Mim yenye Sukun................................. 26**

**Darasa ya (8) Madda: Sehemu ya (1): Aina za Madda za Asili.......... 30**

**Darasa ya (9) Madda: Sehemu ya (2): Madda kwa sababu ya Hamza. 35**

**Darasa ya (10)Madda: Sehemu ya (3): Madda kwa sababu ya Sukun.. 38**

**Darasa ya (11)Makhaarij za herufi (1)............................................... 44**

**Darasa ya (12)Makhaarij za herufi (2)............................................... 47**

**Darasa ya (13)Sifa za herufi (1)..................................................... 52**

**Darasa ya (14)Sifa za herufi (2)..................................................... 57**

**Darasa ya (15)Id'gham zenye kufanana, Zilizojanisiwa na zenye Kukaribiana............................................................................ 61**

**Darasa ya (16)Herufi za Nooraniyyah............................................... 65**

**Darasa ya (17)Attafkheem na Attarqeeq........................................... 67**

**Darasa ya (18)Kukutanika herufi mbili zenye sukun............................ 71**

**Darasa ya (19)Kusimama na Kuanza (1)........................................... 74**

**Darasa ya (20)Kusimama na Kuanza (2)........................................... 77**

**Darasa ya (21)Vituo vifupi vitano, na Alif saba.................................. 85**

**Matanabahisho.......................................................................... 87**

**Takbeer na Kukhitimisha Qur'an.................................................... 92**

بسم الله الرحمن الرحيم

DARSA YA KWANZA

# تـــلاوة القرآن

# USOMAJI (BORA) WA QUR’AN

قال تعالى:

(1) → وَرَتِّلِ الْقُرْآنَ تَرْتِيلًا ﴿٤﴾

(2) → كَذَٰلِكَ لِنُثَبِّتَ بِهِ فُؤَادَكَ ۖ وَرَتَّلْنَاهُ تَرْتِيلًا ﴿٣٢﴾

MAANA YA HIZO AYA ZA JUU:-
AYA(1) Amesema Mwenyezi – Mungu Mtukufu: Na soma Qur’ani vilivyo (Surat Muzamil).

AYA(2) Kama hivi ili tuuthabitishe moyo wako (yaani tuutie nguvu moyo wako; kwa hizo aya mpya zinazoteremka wakati baada ya wakati) na tumeipanga kwa vizuri (Surat-el-Forqan).

Amesema Mtume (S.A.W):

> Mwenyezi-Mungu Anapenda isomwe Qur’ani kama ilivyoteremshwa.

قال رسولُ الله صلى الله عليه وسلم:

((إِنَّ اللهَ يُحِبُّ أَنْ يُقْرَأَ الْقُرآنُ كَمَا أُنْزِلَ))

Uzuri ulioje tukiisoma Qur’ani kama ilivyoteremshwa kwa Mtume wetu Muhammad (S.A.W) Na kama Alivyoisoma Mtume Mtukufu kwa Masahaba wake kwa upole na taratibu na kuipa kila herufi haqi yake ipasavyo kutokana na Madda na Ghunna na Idh’haar na Id’gham na Tafkhim na Tarqeeq na mengineyo.
(Tutaeleza hayo juu tutakapofikia maelezo yake).

Kwa hivyo Wataalamu wameweka qawaida (misingi) na Kanuni za usomaji sahihi wa Qur’ani, ili kuhifadhi kitabu cha Mwenyezi-Mungu na kuogopa yasitokee makosa na wameona kwamba

mafunzo ya qawaid za usomaji na uendelezaji bora ni fardhi kifaya juu ya Waislamu yaani wakijifunza baadhi yao inatosha wanasameheka waliobaki; ama kufuata qawaid (misingi) zake katika kusoma maneno ya Qur'ani ni fardhi ayn, yaani lazima kwa kila msomaji wa kitabu cha Mwenyezi-Mungu. Kama alivyosema Mtaalamu mkubwa Ibn –el- Jazary:

والأَخذُ بالتجويدِ حَتمٌ لازمُ      من لم يجوّدِ القـُـرآن آثمُ

لأَنَّـــهُ بـــهِ الإِلٰـــه أَنـــزَلا      وهٰـــكذا منْـــهُ إِلينا وَصَلا

Kwa ufupi asiyesoma Qur'ani barabar na kuzitamka herufi zake sawa sawa (yaani akatamka Kaf (ك) penye Qaf (ق) au akatamka sin (س) penye Ssad (ص) na kadhalika, anapata dhambi).

Zimegaiwa njia za Usomaji wa Qur'ani namna tatu na zote zinafaa:

1. ATTARTEEL: (الترتيل) NI USOMAJI WA POLE POLE NA UTULIVU NA KUZIPA HERUFI HAQI YAKE (yaani kuzitamka vizuri) KUTOKANA NA SEHEMU MBALI MBALI ZA KINYWA NA MIDOMO NA SIFA ZAKE NA YAPASAYO KUTOKANA NA MADDA NA GHUNNA NA MENGINEYO.

2. AL-HADR: (الحـــدر) USOMAJI WA MBIO MBIO PAMOJA NA KUZINGATIA HUKUMU ZA USOMAJI AMBAPO ZISIFUPISHWE MADDA NA ZIHIFADHIWE GHUNNA NA MENGINEYO.

3. ATTADWEER: (التدوير) NAO NI USOMAJI WA KATI KWA KATI BAINA YA USOMAJI WA MBIO MBIO NA USOMAJI WA TARATIBU.

Kwa hivyo tunaona kuwa Hukumu za usomaji lazima kuhifadhiwa katika kila hali au namna au njia za kusoma Qur'ani.

Na ujuwe ewe ndugu Muislamu kuwa usomaji sahihi unasaidia kufahamu kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu ambapo usomaji wa mbio mbio haumsaidii mwenye kusoma au msikilizaji kufahamu yaliyokusudiwa katika Ayaat -el- Bayyinaat (Aya zilizobainishwa).

## TUJIKUMBUSHE

1. Kujifunza Hukumu za Tajweed (yaani kujua hukumu kutokana na Id'gham na Ikhfaa na mengineyo) ni fardhi kifaya (yaani wakijifunza baadhi ya watu inatosheleza watu wote) lakini kuitumia Qur'ani na kuifuata ni fardhi ayn (yaani lazima) kwa watu wote, nayo ni mafunzo matukufu kabisa kushikamana nayo mafunzo au elimu hiyo ya Qur'ani kikiwa kitabu cha Mola wa viumbe wote.

2. Njia za usomaji ulio sahihi ni tatu :-

a) <u>Attarteel:</u> kusoma kwa taratibu na utulivu na kuzipa herufi zote haqi yake (yaani kuzitamka vizuri).
b) <u>Al Hadr:</u> usomaji wa mbio mbio pamoja na kuzingatia Hukumu za Tajweed.
c) <u>Attadweer:</u> usomaji wa kati kwa kati (si mbio, wala pole pole).

DARSA YA PILI

# الاستعاذة والبسملة

**قال اللهُ تعالى:**

فَإِذَا قَرَأْتَ ٱلْقُرْءَانَ فَٱسْتَعِذْ بِٱللَّهِ مِنَ ٱلشَّيْطَٰنِ ٱلرَّجِيمِ ﴿٩٨﴾ (النحل)
إِنَّهُۥ مِن سُلَيْمَٰنَ وَإِنَّهُۥ بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ﴿٣٠﴾ (النمل)

Ukianza kusoma Qur'ani uanzie: Audhu Billahi mina shayttani Rrajim; tena Bismillahi Rrahmani Rrahim. Mwenyezi – Mungu Ametuamrisha hivyo tukisoma Qur'ani; ili tutake kulindwa na kuhifadhiwa na Mwenyezi–Mungu kwani tunaposoma tunakuwa chini ya ulinzi na hifadhi ya Mwenyezi–Mungu na shetani anaruka na kukimbia akisikia inasomwa Qur'ani. Vile vile Mwenyezi Mungu Anatuhifadhi na riya (kujionyesha) na kupoteza ujira na thawabu kwa sababu ya wasiwasi wa shetani na kedi yake.

Namna za Istiadha ni nyingi lakini zilizo maarufu ni:-

((أَعوذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْم))

و ((أَعُوذُ بِاللهِ السَّمِيْعِ العليمِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ))

Iliyochaguliwa zaidi ni namna ya mwanzo.
Ukisoma kwa siri basi na Istiadha iwe kwa siri na ukisoma dhahiri (mbele za watu) na Istiadha iwe dhahiri.
Ikiwa kusoma kwa zamu baina ya watu isomwe Istiadha kwa siri ikifika zamu yako; ili kusoma kuwe kunaendelea (pasiwe kukatwa kwa Istiadha). Kukisitishwa kusoma kwa kula au kazi nyengine irudishwe Istiadha (mkianza tena).

Ama Bismillahi; tumeamrishwa tuanzie kila kitu kwa hivyo imetajwa katika kuanzia kila Sura katika Qur'ani isipokuwa Surat Attawba (براءة) kwa ajili Bismillahi ni amani na katika Sura hii imeachwa kwa kuvunja ahadi makafiri.

Bismillahi ni Aya iliyoteremshwa kupambanua baina ya Sura na Sura; na imekubaliwa kuwa ni sehemu ya aya katika Surat – Annaml.

Kwa Istiadha na Bismillahi katika mwanzo wa Sura zina hali nne na zote zinafaa:-

1. Kuendeleza pamoja Istiadha na Bismillahi na mwanzo wa Sura. Mfano:-

((أَعُوذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللهِ الرحْمَــٰـن الرَّحِيمِ الْحَمْدُ للهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ))

2. Kuzikata zote; yaani kusimama baada ya Istiadha; na baada ya Bismillahi, tena ukaianza Sura. Mfano:-

((أَعُوذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمْ * بِسْمِ اللهِ الرحْمَــٰـن الرَّحِيمْ * قُلْ هُوَ اللهُ أَحَدْ))

3. Kuendeleza Istiadha na Bismillahi ukasimama tena ukaanza Sura. Mfano:-

((أَعُوذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللهِ الرحْمَــٰـن الرَّحِيمْ * قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَــلَقْ))

4. Kusimama baada ya Istiadha na kuendeleza Bismillahi pamoja na mwanzo wa Sura. Mfano:-

((أَعُوذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمْ * بِسْمِ اللهِ الرحْمَــٰـن الرَّحِيمِ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلنَّاسْ))

Ama ikiwa tunasoma Sura na tukaimaliza na tukataka kuanza Sura mpya tunatumia hali tatu katika zile nne:

1. Kuendeleza aya ya mwisho wa Sura pamoja na Bismillahi ya Sura ifuatayo na tukafuatisha aya ya kwanza, kama:

((فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ مَّأْكُولٍ بِسْمِ اللهِ الرحمــٰـنِ الرَّحِيمِ لِإِيلاَفِ قُرَيْشْ)).

2. Kusimama mwisho wa Sura na kusimama baada ya Bismillahi na kuanza Sura mpya:

((وآمَنَهُم مِّنْ خَوْفْ * بِسْمِ اللهِ الرحمــٰـن الرَّحِيمْ * أَرَأَيْتَ الَّذِي يُكَذِّبُ بِٱلدِّينْ))

3. Kusimama kwenye mwisho wa Sura na kuendeleza Bismillahi na mwanzo wa Sura ifuatayo:

((وَيَمْنَعُونَ الْمَاعُونْ * بِسْمِ اللهِ الرحمٰن الرَّحِيمِ إِنَّا أَعْطَيْنَاكَ الْــكَوْثَرْ))

Ama hali ya nne nayo ni kufikisha mwisho wa Sura na kuendeleza na Bismillahi na kusimama tena ukaanza Sura ifuatayo haifai; kwa sababu msikilizaji asije akafikiri Bismillahi ni aya ya mwisho wa Sura iliyotangulia.

## TUJIKUMBUSHE

1) Istiadha na Bismillahi na mwanzo wa Sura ina hali nne na zote zinafaa.
i) Kuungisha zote.
ii) Kuziweka mbali mbali zote.
iii) Kuunganisha Istiadha na Bismillahi ukasita.
iv) Ukaunganisha Bismillahi na mwanzo wa Sura.

2) Hakika Bismillahi ni baina ya Sura mbili. Zina hali tatu:-
i) Kuunganisha zote (pasina kusita).
ii) Kusita baina ya zote.
iii) Kuunganisha Bismillahi na mwanzo wa Sura.
Inakatazwa kuunganisha Bismillahi na mwisho wa Sura iliyotangulia na ukasita kwenye mwanzo wa Sura ya pili.

DARSA YA TATU

# اللامـــــــــات

# وَهَمْزَةُ الوَصْل

- ❖ لام التعريف: أ- الشمسية ب- القمرية
- ❖ لام الفعل

**قال الله تعالى:**

ٱلرَّحْمَٰنُ ﴿١﴾ عَلَّمَ ٱلْقُرْءَانَ ﴿٢﴾ خَلَقَ ٱلْإِنسَٰنَ ﴿٣﴾
عَلَّمَهُ ٱلْبَيَانَ ﴿٤﴾ ٱلشَّمْسُ وَٱلْقَمَرُ بِحُسْبَانٍ ﴿٥﴾
وَٱلنَّجْمُ وَٱلشَّجَرُ يَسْجُدَانِ ﴿٦﴾

## LAMU

Hatuna Lamu namna hii katika lugha ya Kiswahili. Lamu hii hutumiwa katika lugha ya Kiarabu kuarifisha (kujulisha) kitu kisichojulikana k.m. ukisema kitabu (ni kitabu chochote) lakini baada ya kujulikana hutiwa 'Lamu' Alkitab (kitabu maalumu).

Zipo Lamu namna mbili:

(1) LAMU YA KUARIFISHA (kujuvya) ١- لام التعريف

(2) LAMU YA KITENDO ٢- لام الفعل

Tukiangalia Aya Tukufu hapo juu, tutaona majina yaliyoarifishwa kwa kutiwa (AL) nayo ni:

( الرَّحمٰن- الْقرآن- اَلإِنسان- الْبيان- الشَّمس- الْقمر- النَّجم- الشَّجر).

Tunaona kuwa Lamu katika (ال) ya kuarifisha imedhihirika kwa uwazi kabisa maneno haya:

(اَلْقرآن - اَلإِنسان - اَلْبيان - اَلْقمر).

Ukiyasoma unaitamka (AL) kwa uwazi k.m. Al-Qur’an.
Ambapo katika maneno yaliyobakia Lamu imeingizwa katika herufi inayofuata na kudhihirika shadda juu ya herufi hiyo. Muingizo huu unaitwa إدْغَــام katika mafunzo ya Qur’an.

Arrahman – Ash’shams n.k. (اَلرَّحمن– اَلشَّمس– اّلنَّجم– اَلشَّجر).

Kwa hivyo Maulamaa wamechukua tamko (القمر) kuwa mfano; juu ya kudhihirika Lamu na wakaiita LAMU AL QAMARIYA

اللام القمرية

na wakachukua tamko (الشَّمس) kuwa ni mfano wa Id'gham ya Lamu na kuiita LAMU ASHSHAMSIYA اللام الشمسية.

Katika kuelezea muungano wa Lamu (au kushikamana) Lamu na herufi za Alfabeti katika mianzo ya majina inatubainikia kwamba Lamu inawajibika kudhihirika ikishikamana na herufi kumi na nne zifuatazo:

(الهمزةُ والباءُ والغينُ والحاءُ والجيم والكافُ والواوُ والخاءُ
والفاءُ والعينُ والقافُ والياءُ والميمُ والهاءُ)

{أ – ب – غ – ح – ج – ك – و – خ – ف – ع – ق – ي – م – ه }.

Wataalamu wameziweka pamoja (wepesi wa kufahamika) katika maneno haya:

(إبغِ حجَّكَ وخف عقِيمَه) (na pia wepesi kuhifadhika).

Na inabidi LAMU kuingizwa katika herufi inayofuata ikiwa mojapo ya herufi kumi na nne zilizobaki nazo:

(الطاءُ والثاءُ والصادُ والراءُ والتاءُ والضادُ والذالُ والنونُ
والدالُ والسينُ والظاءُ والزايُ والشينُ واللامُ)

{ط ،ث، ص، ر، ت، ض، ذ، ن, د، س، ظ، ز، ش، ل}.

Na Wataalamu wameziweka katika beti ya ushairi ufuatao, mwanzo wa kila neno:

طِبْ ثم صِلْ رَحِماً تَفُزْ ضِفْ ذا نِعَمْ
دَعْ سُوءَ ظَنّ زُرْ شَرِيفاً لِلكَرَمِ

Inajulikana kwamba LAMU ASHSHAMSIYA اللاَمَ الشَّمسيةَ na LAMU AL QAMARIYA اللاَمَ القمرية hutiwa hassa katika majina.

Yanapokuwa majina ya vitu visivyojulikana kwanza huitwa kwa Kiarabu التنكير yaani kutojulikana. Kwa hivyo vikisha kujulikana hutiwa Lamu zilizoanziwa nayo majina na huwa wakati huo maalumu na huitwa التعريف.

Ama Lamu za vitendo inapasa kudhihirishwa daima katika herufi zote k.m.

(جَعَلْنَا – ظَلَّلْنَا – وَلْتَكُنّ – قُلْ هُوَ اللهُ أَحَدٌ).

Isipokuwa herufi mbili Ra na Lamu (ر+ل) اللام والراءُ k.m. (قل لّو) ukiangalia utaona pana muingiliano wa Lamu ya kwanza kuchanganyika na Lamu ya pili na muingiliano huu huitwa Id'gham, na hapa ilivyokuwa herufi zote mbili ni namna moja huitwa Id'gham yenye kufanana:-

Kwa Kiarabu huitwa ⟶ إِدغام مُتَمَاثِلَيْن

Namna ya pili ikiwa herufi zinakaribiana matamshi kama herufi ya (ر+ل) Lamu na Ra k.m. (وقلْ ربِّ زِدْنِي عِلْما)

zikiingiana huitwa Id'gham Mutaqaribaini:- إدغام مُتَقَارِبَيْن

Tukichungua hizi Lamu, hassa zile zinazoanzia majina utaona hazikuanzia Lamu peke yake bali mwanzo wake kuna ALIF juu yake kissad (ص) kidogo. Alif hii huitwa HAMZATEL-WASL

## همزة الوصل

Imeitwa kwa jina hilo kwa sababu huwasilisha (huendeleza) kutamka na herufi yenye sukun na ni njia ya kumakinisha kutamka kwa hiyo Hamzatel - wasl.

Ama katika mfano tuliyoiyona katika mwanzo wa darsa hii zimetiwa katika majina tu nazo:

ٱلْقُرْءَان ⟵ Hamzatelwasl

Lam Al- Qamariya

ٱلرَّحْمَٰن ⟵ Hamzatelwasl

Lam Ashhamsiya

Zinopokuwa na Lamu Alqamaria huwasilishiwa nayo na kuwa AL. Ama Lamu Ashshamsiya huwa haitamkwi huingizwa kwenye herufi baada ya Lamu.

## HAMZATEL-WASL

Hamzatel-Wasl hudhihirika kutamkwa kwake inapoanzia mwanzo wa neno, lakini huwa haitamkwi ukiwasilisha maneno (yaani ukiendelea kusoma) kwa mfano:

Tunasoma Annajm, tunaitamka (Hamzatel-wasl). ٱلنَّجْمُ

Lakini tukiendelea kusoma hatuitamki. Kwa mfano:

خَلَقَ ٱلإِنسَٰن وَٱلنَّجْمُ وَٱلشَّجَرُ يَسْجُدَانِ

Au likianza neno kabla yake au herufi haitamkwi (Hamzatel-Wasl) Tunasoma 'Khalaqal-Insan' 'wannajmu' 'washshajaru' Hatuzitamki lakini zinaandikwa.

Hamzatel-Wasl (kama tulivyokwisha kuona) hutiwa katika majina, bali pia hutiwa kwenye vitendo na Herufi (kama juu) waw وَ.

Ama zikitiwa katika vitendo huwa kama hivi ifuatavyo:

Vitendo vilivyokwisha kupita zamani:

Surat ص Aya ya (6) ﴿ٱنْطَلَق﴾ من قوله تعالى: ﴿وٱنْطَلَقَ ٱلملأُ مِنْهُم﴾

Ukisoma peke yake neno moja likianzia Hamzatel-Wasl tunatamka (Inttalaqa) lakini tukianzia neno au herufi na kuendelea tunasoma (Wantalaqal-malau) (Hatuzitamki Hamzatel-Wasl).

Vile vile: Surat Annur Aya ya (11)

﴿ٱسْتَحَقّ﴾ من قوله تعالى: ﴿على أَنَّهُمَا ٱسْتَحَقَّا إِثْماً﴾.

Ama herufi haziingizwi katika Hamzatel - wasl ila huwa na zile Lamu Al-qamariya au Ashshamsiya k.m. Herufi ni Inna na Wa (إِنَّ، وَ) Surtel Ahzaab Aya ya 5

﴿إِنَّ ٱلمُسْلِمِيْنَ وَٱلمُسْلِمَاتِ وٱلمُؤْمنينَ وَٱلمُؤْمِناتِ وَٱلقَانِتِينَ وَٱلقَانِتَاتِ﴾.

## HUKUMU ZAKE

1) Hutiwa Fat'ha Hamzatel-Wasl zikiingizwa kwenye LAMU ATTAARIF kwa mfano:

لام التعريف: { ٱلأرض، ٱلْبَحر، ٱلْجبال، ٱلسماء، ٱلشّكور، ٱلّذي }.

Tunasoma:

"ALhamdulillahi" ٱلْحمْدُ لله رَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ

"Arrahmani" ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَحِيمِ

2) Hutamkwa Hamzatel-Wasl kwa kasra zinapoanziwa na kitendo ambacho herufi ya tatu yake ina fat'ha au kasra au kikiwa asili ya kitendo kilichopita (مصدر فعل الماضي) k.m.

i) Vitendo ambavyo herufi ya tatu vina kasra

﴿ٱهْدِنَا الصِّرَاط المُسْتَقِيْم، ٱرْجِعْ إليهم، ٱتَّبِعْ ما أوْحِي إليكَ من ربك﴾.

ii) Vitendo ambavyo herufi ya tatu vina fat'ha

﴿ ٱسْتَحْوَذَ عليهمْ الشيطانُ، ٱسْتَجِيْبُوا لربّكم﴾.

Zinatamkwa kwa kasra "Ihdina - Istah'wadh n.k."

3) Hutiwa Hamzatel-Wasl pia kasra ikiwa herufi ya tatu ya kitendo chake kina kasra kwa mujibu wa haraka yake ya asili (ilikuwa kasra) tena ikabidi kugeuzwa dhamma ili zisikutane sukun mbili katika vitendo hivyo.

Navyo ni vitendo hivi: 1 2 3 4

﴿ٱئْتُوا﴾ ﴿ٱقْضُوا﴾ ﴿ٱبْنُوا﴾ ﴿ٱمْشُوا﴾

Asili yake vilikuwa:

(ٱيْتِيُوا) (ٱقْضِيُوا) (ٱبْنِيُوا) (ٱمْشِيُوا)

(i) Utaona ( ـشِـ) sheen ina kasra na (ـيُـ) ina dhamma tena ikahamishwa haraka ya ( ُ ) dhamma ikapelekwa kwenye sheen ikawa ( ـشُـ) (badala ya ـشِـ) ikaondoshwa ( ـيـ) ili kuepukana kukutana sukun mbili kama ilivyothabitishwa katika Qawaid za Lugha ya Kiarabu kwamba zikikutana sukun mbili hapana buddi na kuondolewa mojawapo, ama kuondolewa herufi ya mwanzo iliyo na sukun au kuitia haraka (ama fat'ha, ama dhamma au kasra) badala ya sukun

na ikawa "ٱمْشُوا" na kadhalika maneno yote yaliyobakia juu (Neno la 2+3+4).

(Angalia: Tutaeleza zaidi kukutana sukun mbili katika darsa ijayo).

(ii) Hutamkwa kwa Dhamma inapoanzia Hamzatel-Wasl ikiwa herufi ya tatu ya kitendo cha kuamrisha ina dhamma ya lazima (ya maumbile) nayo ni dhamma ya asili. Mifano:

Zinasomwa "Udhkurni" ٱذْكُرْنِي عِندَ رَبِّكَ

"Ut'lu" ٱتْلُ مَا أُوحِيَ إِلَيْكَ

4) Huachwa Hamzatel-Wasl katika kuitamka tu! Lakini huandikwa. Unapoendelea kusoma, kwa ajili ya kuwepo harufi yenye sukun kwenye herufi iliyo kabla yake, kwa wakati huo, huwa haina haja na kuitamka Hamzatel-Wasl. Kwa mfano
Suratel Qiyama, Aya 14

Tunasoma "Balil'insanu ..." - بَلِ ٱلإِنسَٰنُ عَلَىٰ نَفْسِهِ بَصِيرَةٌ

Suratel Hujuraat, Aya10
Tunasoma "Innamal'muuminuna"

إِنَّمَاٱلْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ فَأَصْلِحُواْ بَيْنَ أَخَوَيْكُم

Baada ya kujifunza Hamzatel-Wasl na kuona inavyoandikwa ( ٱ ). Kuna Hamza nyengine iitwayo Hamzatul-Qatt'i

"همزة–القَطْعِ"

Nayo inatamkwa na kuthibitika katika hali zote hata ukiendelea kusoma. Nayo huandikwa Hamza juu ya Alif ( أ ). Mifano:

Surat Al Imran Aya 7 ﴿ إِذْ قَالَتِ ٱمْرَأَتُ عِمْرَانَ ﴾

Surat el Balad Aya 18 ﴿أُولَـٰئِكَ أَصْحَٰبُ ٱلْمَيْمَنَةِ ﴾

Surat Fajr Aya 19 ﴿ أَكْلاً لَّمًّا ﴾

## TUJIKUMBUSHE

Inapasa kudhihirika Lamu Al-Qamariya ikiangukia kabla ya herufi kumi na nne zilizowekwa kwenye maneno haya:

( إِبغ حجّك وخف عقيمه)

yaani

{ أ، ب، غ، ح، ج، ك، و، خ، ف، ع، ق، ي، م، ه }.

Na inapasa patokee Id'gham ya Lamu Ashshamsiya (yaani Lamu kuingizwa katika herufi inayoifuata na kukazwa kwa kutiwa shadda) katika herufi zilizobakia nazo:

{ ط، ث، ص، ر، ت، ض، ذ، ن، د، س، ظ، ز، ش، ل }

Ama Lamu ya kitendo inapasa kudhihirika daima katika herufi zote ispokuwa herufi mbili tu katika hizo nazo ni Lamu na Ra(ل+ر) inabidi ziingizwe katika herufi zinazozifuata herufi hizo mbili; Lamu na Ra. Yaani patokee Id'gham.

### HAMZATEL–WASL

Hudhihirika kutamkwa kwake inapoanzia mwanzo wa neno, lakini haitamkwi ukiwasilisha maneno (yaani ukiendelea kusoma)

Mfano: Alhayawan, Alkhair n.k. ٱلْحيَوانُ، ٱلْخيْرُ، ٱلْعلِيْمُ، ٱلْغفُورُ

Maneno haya yameanzia Hamzatel–Wasl na Lamu Attaarif. Lakini ukiendelea kusoma Hamzatel–Wasl hazitamkwi.

Unasoma 'Limanir'tadha' unaiacha ﴿ولاَ يَشْفَعُونَ إِلاَّ لِمَنِ ٱرْتَضَى﴾ Hamzatel–Wasl.

### Hukumu Zake

1. Hutamkwa kwa Fat'ha zikiwa kwenye LAMU ATTAARIF (ٱلزُّجَاج)
2. Hutamkwa kwa Kasra zinapoanzia vitendo ambavyo herufi ya tatu ya vitendo hivyo vina Kasra au Fat'ha ﴿ ٱتَّبِعْ مَا أُوحِيَ إِلَيْكَ مِنْ رَّبِّكَ ﴾
3. Hutamkwa kwa dhamma ikiwa herufi ya tatu ya kitendo cha kuamrisha ina dhamma ya asili ﴿ٱتْلُ مَا أُوحِيَ إِلَيْكَ مِنَ الْكِتَابِ﴾

4. Huachwa Hamzatel–Wasl kuitamka tu, lakini huandikwa, unapoendelea kusoma na pakiwepo herufi yenye sukun kwenye herufi ya kabla yake - ﴿إِنِ ٱرْتَبْتُمْ﴾.

HAMZATEL-QATT'I ( أ )

Alif nyengine ambayo inaandikwa juu yake Hamza nayo ni

'همزة–القطع '

Nayo ni thabiti katika hali zote inatamkwa hata ukiendelea kusoma.

Suratel Insaan Aya ya 4 ﴿إِنَّا أَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ سَلاَسِلَ وَأَغْلاَلاً وَسَعِيرًا﴾

Suratel Qiyama Aya ya 1 ﴿ لاَ أُقْسِمُ بِيَوْمِ الْقِيَامَةِ﴾

DARSA YA NNE

# النون الساكنة والتنوين: الاظهار

قال الله تعالى:

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

إِنَّآ أَعۡطَيۡنَٰكَ ٱلۡكَوۡثَرَ ١ فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَٱنۡحَرۡ ٢

إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ ٱلۡأَبۡتَرُ ٣

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

هَلۡ أَتَىٰكَ حَدِيثُ ٱلۡغَٰشِيَةِ ١ وُجُوهٞ يَوۡمَئِذٍ خَٰشِعَةٌ ٢

عَامِلَةٞ نَّاصِبَةٞ ٣ تَصۡلَىٰ نَارًا حَامِيَةٗ ٤ تُسۡقَىٰ مِنۡ عَيۡنٍ ءَانِيَةٖ ٥

## NUNI YENYE SUKUN NA TANWEEN -(1) AL IDH'HAAR

Hapana budi kwanza kujua maana ya "Idh'har" kwa lugha ya Kiarabu maana yake 'kubainika' (yaani kuonekana wazi wazi) lakini katika mafunzo ya kusoma Qur'ani maana yake: Kuitoa herufu kwenye matokeaji yake ambako kunaitwa "Makh'raj" (kwa Kiarabu) bila ya 'Ghunnah" (nayo ni sauti inayotokea puani unapoisoma, tunasema Fulani anasema kipuani yaani sauti inatokea puani) katika herufi iliyodhihirika.

Sehemu za matokeaji herufi (yaani Makharij) zilizo kubwa ni tano nazo ni:

(1) Al-jawf ni sehemu ya ndani kabisa ya kinywa baina ya koo na ndani ya kinywa

(2) Al Halq - ni koo

(3) Ulimi

(4) Midomo

(5) Sauti inayotokea puani- Al Khaishum

Ni hizi kwa Kiarabu:

مخارجْ الحروف الرءيسية وهي:

الجوفُ، الحلقُ، اللسانُ، الشفتانِ، الخيشومُ

Hatuna budi mwanzo tujue NUNI iliyotiwa sukun ( نْ ) na Tanwin kama tunavyosoma fat'hatein, kasratein, dhammatein kama hivi ( ً ٍ ٌ ).Tukisema Nuni iliyotiwa sukun ina maana kuwa haina haraka. Hiyo juu haina fat'ha wala kasra wala dhamma bali imetiwa sukun juu yake. Hali kadhalika Tanwin ni nuni iliyotiwa sukun inaambatana na jina ukiendelea kusoma; na inakua haipo katika kuiandika au kusimama k.m. (yaani kwa mfano):-

( رسولٌ – رسولاً – رسولٍ )

Tunaposoma huku tunaendelea bila ya kusita ni:

Rasulun, Rasulan, Rasulin: - ( رسولُن – رسولَن – رسولِن )

Lakini tukisimama au tukiandika hatuandiki hivyo juu.
Tunaposita yaani pakiwapo alama ya kusimama tunasoma:

Rasul au Rasulaa au Rasul - (رسولْ – رسولا – رسولْ),

pia ikiwa mwisho wa Aya au penye alama ya kusimama.
Tukirejea mwanzo wa darsa hii au maelezo haya, katika Aya ya kwanza Surat Kawthar tunaona katika Aya ya pili neno ( وَٱنْحَرْ )
Imo nuni iliyotiwa sukun ambayo inadhihirika pasina kuikaza hiyo nuni inatamkwa kwa ncha ya ulimi inayogusa sehemu ya juu ya kinywa.

Katika mfano wa pili katika Surat-el-Ghashiya Aya ya 2 tunaiona Tanwin inayobainisha nuni yenye sukun (يومئذٍ خَاشِعَةٌ)

vile vile katika Aya ya 4 na ya 5. (ناراً حامية) – (عينٍ آنية)

Inadhihirika Nuni yenye sukun na Tanwin inapoangukia baada yao moja ya herufi hizi sita, nazo ni:-

Hamza na Ha na Ayn na Hha (ح) na Ghayn na Kha kama hivi kwa Kiarabu الهمزة والهاءُ والعين والحاء والغين والخاءُ.

Hamza yenyewe inakuwa juu ya alif ( أ ).

Mtaona juu kwenye mifano: Yawmaidhin.. herufi inayofuata (خ) khashiah. Tanwin ya pili (Naaran) herufi inayofuata ni Hha (ح) na mfano wa tatu (Aynin) herufi inayofuata ni hamza juu ya alif lakini

imetiwa (madda) badala ya Hamza ( آ ). Hapana tafauti ikiwa nuni na herufi za Idh’har (Hizo 6 tulizozitaja kabla na tutakuwa tukiziita kwa Kiarabu ni wepesi zaidi ni juu yetu kujifunza maana yake) zikiwa katika neno moja au maneno mawili. Herufi hizi za Idh’har vile vile zinaitwa herufi za kooni kwa sababu zinatamkwa kutokea kooni.

Ifuatayo mifano itakayoonyesha kwanza Nuni yenye sukun yenye kufuatwa na herufi za Idh’har katika neno moja na baadaye katika maneno mawili tena Tanwin inayofuatwa na herufi za Idh’har katika jedwali ifuatayo kwa Kiarabu (kuanzia kulia kuja kushoto) katika maneno ya Qur’ani tukufu.

| (3) | (2) | (1) | Herufi za Idh’har | |
|---|---|---|---|---|
| –كلٌ آمن | –ومنْ أَعْرَضَ | يَنْأَوْنَ | الهمزةُ: | ( أ ) |
| –فريقاً هدى | –منْ هَاد | يَنْهَوْنَ | الهاءُ: | ( ه ) |
| –حكيمٌ عليم | –مَن علم | أَنْعَمْتَ | العينُ: | ( ع ) |
| –منْ حكيمٍ حَمِيْد | –مَنْ حادَّ | وَانْحَرْ | الحاءُ: | ( ح ) |
| –ماءٍ غَيْرِ آسِنٍ | –منْ غَلَّ | فَسَيُنْغِضُونَ | الغينُ: | ( غ ) |
| –يومئذٍ خَاشِعةٌ | –هل منْ خالقٍ | والمنْخَنِقَةُ | الخاءُ: | ( خ ) |

Maelezo mafupi juu ya jedwali:

(1) Neno moja يَنْأَوْنَ: nun yenye sukun ‘yan’ imefuatiwa na herufi ya Idh’har ( أ ).

(2) Maneno mawili –وَمَنْ أَعْرَضَ : waman aa’radha (1) (2)
nun yenye sukun na imefuatiwa na herufi ya Idh’har

(3) Tanwin فَرِيقاً هُدى Fariqan imefuata herufi ya Idh’har (**ه**)

## TUJIKUMBUSHE

1. ATTANWEEN: Nun yenye sukun unaitamka mwisho wa jina ukiendelea kusoma na huwa haipo ukiiandika au ukisimama.
2. Al-IDH'HAAR: Kilugha maana yake mbainisho na katika mafunzo ya Qur'ani (inayoitwa ISTTILAAHAN اصطلاحًا) ni kuitoa herufi kwenye makhraj yake bila ya Ghunnah.
3. Herufi za Idh'haar kwa mujibu wa Nun yenye sukun na Tanween ni:
   Hamza – Ha – Ayn – Hha – Ghayn – Kha, na Wataalam wamezikusanya herufi za mwanzo za maneno haya:

   أخي هاك علماً حازه غير خاسر

   Kwa wale wanaotaka kuzihifadhi na wepesi kuzikumbuka.

DARSA YA TANO

# النون الساكنة والتنوين: الإدغام

قال الله تعالى:

فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا

يَرَهُۥ ﴿٧﴾ وَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُۥ ﴿٨﴾

(الزلزلة)

وَيْلٌ لِّكُلِّ هُمَزَةٍ لُّمَزَةٍ ﴿١﴾ ٱلَّذِى جَمَعَ مَالًا وَعَدَّدَهُۥ ﴿٢﴾

(الهمزة)

## NUNI YENYE SUKUN NA TANWEEN-(2) AL-ID'GHAM

Kabla ya kuingia katika darsa yenyewe hatuna budi kujuwa maana ya neno hilo "ID'GHAM". Kwa lugha ya Kiarabu maana yake kuingiza kitu katika kitu kuwa kimoja. Amma katika kujifunza kusoma Qur'an ni kukutanika herufi yenye sukun na herufi yenye haraka (ama fat'ha, ama kasra au dhamma) na ukatamka kama kwamba herufi moja yenye mkazo kwenye herufi ya pili:-

Herufi ambazo zinaingiana ndani yake NUNI YENYE SUKUN NA TANWEEN ni herufi sita nazo:

Ya – Ra – Mim – Laam – Waw na Nun

النون – الواو – اللّام – الميم – الراء – الياء

Hukusanyishwa pamoja na kuzisoma kama neno moja YARMALUN 'يرملون'.

ID'GHAM ina sehemu mbili:

(1) ID'GHAM PUNGUFU, INA GHUNNAH

(2) ID'GHAM KAMILI, BILA YA GHUNNAH

1. Id'gham pungufu imeitwa pungufu kwa kubakia athari ya nuni iliyoingizwa katika herufi ya pili nayo ni ghunnah (sauti ya ghunnah inatokea puani pasina kutumia ulimi!) inayovutika kiasi haraka mbili (nazo ni kiasi cha kufunga vidole viwili vya mkono).

Herufi za Id'gham pungufu ni nne katika zile sita tulizozitaja nazo ni 'Ya' na 'Waw' na 'Mim' na 'Nun'. Tuangalie mithali ya herufi hizo:-

| (2) | (1) | | |
|---|---|---|---|
| وجوهٌ يَّومئذٍ- | مَن يَّقُول: | اليـــاء | Ya |
| حسنةً وَّقِنا- | مِن وَّال: | الوَاوُ | Waw |
| صراطٍ مّستقيم- | مِن مَّالٍ: | المِيْمُ | Mim |
| يَوْمَئذٍ نَّاعِمَة- | عَن نَّفْسٍ: | ألنُونُ | Nun |

Tukianzia 'Ya' ambayo imo katika neno la pili "Yaqulu" ukiyasoma maneno hayo mawili unaisoma kwa sauti inayotokea puani na utaona 'nun' inatamkwa kwa mbali "ma'n' yaqulu" (nimetia nuni ndogo kuonyesha athari yake kwa udogo au mbali. Hutamki 'manyaqulu' (unapotamka hivyo utaona ncha ya ulimi inagusa juu, ni makosa usitumie ulimi kabisa bali itoe sauti ya kipuani). Na kadhalika 'Tanwin' usitamke wujuhun kwa ncha ya ulimi kugusa juu lakini itolee sauti ya puani wujuhunyawmaidhin (nuni itoe kwa mbali). Lakini unaikaza herufi ya pili.

2. Id'gham kamili imeitwa hivyo kwa kutobakia athari ya nuni (katika herufi iliyoingizwa ndani yake nuni.). Herufi zake ni mbili katika zile sita nazo ni 'Lam' na 'Ra' Angalia mifano ifuatayo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| أنداداً لِّيضلوا- | ولم يكن لَّه: | اللامُ | 'LAM' |
| لرؤوفٌ رَّحيم- | من رَّبهم: | الراءُ | 'Ra' |

Id'gham kamili haina ghunna kama ya juu (yaani sauti haitokei puani) unaikaza tu kwasababu kuna shadda katika herufi ya pili.
Tukianzia 'Lam' (baada ya nuni yenye sukun) hatuitamki nuni kabisa inapotea na tunasema 'walam yakullahu'.

Kadhalika mfano wa pili 'Tanween' Hatuitamki Andadan bali nuni inapotea katika tanwin inabakia 'fat'ha' moja tu nayo ni andada kwa hivyo ukisoma unasoma 'Andadalliyudhillu' Anglia hapa 'dh'

si dhal (ذ) bali (ض). Na kadhalika 'Ra' katika mifano ya pili katika jedweli, (haibakii athari ya nuni na unakaza Ra.)
Ukichungua katika mifano yote uliyopewa, inaonyesha kuwa Nuni yenye sukun na herufi za Id'gham hazikutani katika neno moja bali maneno mawili au zaidi. Kwa hivyo pindi zikikutana inakatazwa "Id'gham" na hapo inapasa nuni idhihirike na wakati huo itakuwa 'Idh'haar' na hapana maneno hayo katika Qur'an ila maneno manne tu nayo:-

(دُنْيَا، قِنْوَانٌ، صِنْوَانٌ، بُنْيَانٌ)

Na hukumu yake inaitwa Idh'haaran-Muttlaqa (إظهاراً مطلقا).

Kuna maudhuu mbili pia hazifuati hukumu ya Id'gham yanatakikana kudhihirika nun ndani yake nayo:

( يسٓ وَٱلْقُرْءَانِ ٱلْحَكِيمِ ) و ( نٓ ۚ وَٱلْقَلَمِ وَمَا يَسْطُرُونَ )

Ya'sin: nuni inatamkwa; pia nun wal-qalami; nun inatamkwa.
Pia inalazimika kudhihirisha ghunna kwenye nuni iliyotiwa shadda k.m. In'nna, jahan'nnama - (جهنَّم – إنَّ).

Mifano:-

{إِنَّ بَعْضَ ٱلظَّنِّ إِثْمٌ} {وَظَنَّ أَنَّهُ ٱلْفِرَاقُ} {كَأَنَّهُمْ حُمُرٌ مُّسْتَنفِرَةٌ}

## TUJIKUMBUSHE

1. ID'GHAM: Kilugha ni kuingiza kitu katika kitu.
   Ama katika mafunzo ya Tajweed ya Qur'an ni kuikutanisha (kuiingiza) herufu yenye sukun katika herufu yenye haraka (fat'ha, kasra au dhamma) na unatamka kama kwamba herufi moja yenye mkazo katika herufi ya pili (ile yenye haraka).

2. Herufi za Id'gham na tanween ni sita nazo:

   (الياء و الراء والميم وللام والواو والنون)

   Hukutanishwa pamoja katika neno moja: YARMALUN.

   (يرملون)

3. ID'GHAM inagawika sehemu mbili:
   (i). ID'GHAM PUNGUFU NA YENYE GHUNNAH na herufi zake ni 4: (الياء والواو والميم والنون)
   nazo huweza kukutanishwa katika neno moja na kusemwa YAWMAN (يَوْمَنْ).
   (ii). ID'GHAM KAMILI BILA YA GHUNNAH na herufi zake ni 2 Lamu na Ra (اللام والراء).

4. Inashurutishwa katika Id'gham iwe nun mwisho wa neno la kwanza na herufi ya Id'gham iwe mwanzo wa neno la pili; zikikutanishwa pamoja katika neno moja inapasa kudhihirishwa "الاظهار" mfano:

   (دُنْيَا – قِنْوانٌ – بُنْيَانٌ – صِنْوَانٌ)

   Pia hutoka katika hukumu ya Id'gham katika maneno hayo yafuatayo na inatakikana kuyadhihirisha (yaani kudhihirika nuni) 'الاظهار'

   (يسٓ والقرآن الحكيم) و (نٓ والقلم وما يسطرون)

DARSA YA SITA

# النون الساكنة والتنوين: الإقلاب والإخفاء

**قال الله تعالى:**

لِلَّهِ ٱلْأَمْرُ مِن قَبْلُ وَمِنۢ بَعْدُ (الروم-٤)

فَمَن شَهِدَ مِنكُمُ ٱلشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ (البقرة-١٨٥)

## NUNI YENYE SUKUN NA TANWEEN - IQLAAB na IKH'FAA

Maana ya 'IQLAAB' kilugha ni kugeuzwa ndani nje kama unapovaa kanzu nje ndani. Ama katika Qur'an ni kugeuka nuni yenye sukun na kuwa mim; na kufichika kwake hiyo nuni kwa ghunna kwenye herufi moja tu nayo ni 'Ba' Kiarabu al-bau **الباء**

**الأَمثلةُ: ( أَنْبئهم – أَنْ بورك – كلٌ نفسٍ بِمَا كَسَبَتْ رَهِيْنَة)**

**فتقرأُ ( أَمبئْهُمْ – أَمْ بُورِكَ – كُل نَفْسِمْ بِمَا كَسَبَتْ رَهِيْنَة)**

Husomwa hivi:

Ambiihum – Amburika – Kullu nafsim-bima….

Tuangalie hizo aya mbili juu tutaona neno: **ومن بعد** tumetiliwa mim ndogo juu ya nuni. Maneno yote kama hayo yenye kutiwa mim ndogo juu ya nuni yenye sukun, nuni hupotea na kutamkwa ile mim ndogo. k.m.

Tunaigeuza nuni yenye sukun na kuwa mim. **منْ بعد**

Kwa hivyo tunatamka mimbaadu. Hukumu hiyo huitwa AL-IQLAAB. Na tunaitamka kwa ghunna kwa kukutanisha midomo yako miwili kwa mkazo ili itoke sauti ya ghunna kwa puani. Kwa hivyo herufi ya Iqlaab ni moja tu nayo ni 'Ba' inapokuwa baada ya nuni yenye sukun. Kwa maana nyengine ni tunaigeuza nuni yenye sukun iliyopo kabla ya 'Ba' na kuwa mim yenye sukun vile vile, inayotamkwa kwa ghunna.

Tukiangalia Aya ya pili, tutaona nuni yenye sukun katika neno la mwanzo (فَمَنْ شَهِدَ) na (مِنْكُم) Faman shahida na minkum.

Hutamkwa baina ya Id'gham na Idh'har pamoja na ghunna kiasi cha haraka mbili na huitwa hukumu hii 'IKH'FAA'.

IKH'FAA maana ya kilugha ni kuficha' lakini katika Qur'ani Tukufu ni kutamka herufi katika hali baina ya Idh'har na Id'gham bila ya kuikaza lakini pawepo ghunna katika herufi ya mwanzo. (inabidi tuhifadhi vyema maneno haya kwani tutayatumia hivyo hivyo kwa Kiarabu au tutababaishika tukiyafasiri)

Mifano ya herufi za IKH'FAA inafuatia katika ukurasa ufuatao, utaona katika mstari wa kwanza (kwa urefu) NUNI YENYE SUKUN NA HERUFI YA IKH'FAA katika neno moja. Na mstari wa pili katika maneno mawili na mstari wa tatu ni TANWEEN na herufi ya IKH'FAA.

# HERUFI ZA IKH'FAA

| Mstari (3) | Mstari (2) | Mstari (1) | HERUFI ZA IKH'FAA |
|---|---|---|---|
| عذاباً صعداً | ولمَن صبَر | ينصركم : | (ص)- الصاد |
| بسلامٍ ذلك | مَن ذا | منذر : | ( ذ )- الذال |
| نُطفَةٍ ثُمَّ | من ثمرةٍ | الأُنثى : | (ث)- الثاء |
| كِتابٌ كريم | أفمن كان | منكم : | (ك)- الكاف |
| فصبرٌ جميل | مَن جاءَ | فأَنجيناهُ : | (ج)- الجيم |
| جباراً شقيا | فمن شهد | أنشأناهن : | (ش)- الشين |
| رزقاً قالوا | من قَبْلُ | ينقلب : | (ق)- القاف |
| قيلاً سَلاماً سلاماً | من سُلالَةٍ | الإنسان : | (س)- السين |
| عملاً دون | ومَن دخله | عِندَهُ : | ( د )- الدال |
| بلدةٌ طيِّبَةٌ | من طين | انطلقوا : | (ط)- الطاء |
| نفساً زكية | فإن زَللتم | أَنزلني : | (ز)- الزاي |
| منْ شيءٍ فهو | فإن فاؤوا | أَنفقتم : | (ف)- الفاء |
| جناتٌ تجري | من تحتها | كنتم : | (ت)- التاء |
| قوماً ضالين | مَن ضلَ | منضود : | (ض)- الضاد |
| ظِلاً ظليلاً | من ظهير | فانظر : | (ظ)- الظاء |

Tukichungua tutaona:

| | |
|---|---|
| Herufi sita za Idh'haar | 6 |
| Herufi sita za Id'gham | 6 |
| Herufi moja ya Iqlaab | 1 |
| Herufi kumi na tano (15) za Ikh'faa | 15 |
| Alphabeti ya Kiarabu herufi zake zote ni | = 28 |

## TUJIKUMBUSHE

1. AL-IQLAAB (الإِقلاب) maana yake Kilugha ni kugeuza kitu nyuma mbele (tunatumia mara nyengine neno umevaa kanzu maguluba yaani nje ndani)
   Ama katika mafunzo ya Qur'ani ni kugeuka NUNI YENYE SUKUN AU TANWEEN kuwa MIM na kufichika kwa hiyo NUNI kwa GHUNNAH kwenye herufi moja tu nayo ni BA.

2. AL-IKH'FAA (الإِخفاء) maana yake Kilugha ni 'KUFICHA' lakini katika Qur'an ni KUTAMKA HERUFI BAINA YA IDH'HAAR NA ID'GHAM BILA YA KUKAZA pamoja na kuwepo ghunnah katika herufi ya mwanzo (Ghunnah kwa sauti ya kipuani).
   Na herufi zake za mwanzo zimeekwa pamoja katika beti ifuatayo ili iwe wepesi kuhifadhi:

صِفْ ذَا ثَنًا كَمْ جَادَ شَخْصٌ قَدْ سَمَا

دُمْ طَيِّباً زِدْ فِي تُقىًّ ضَعْ ظَالماً

DARSA YA SABA

## أحكام الميم الساكنة

**قال الله تعالى:**

١ – وَأَنِ ٱحۡكُم بَيۡنَهُم بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ وَلَا تَتَّبِعۡ أَهۡوَآءَهُمۡ (المائدة – ٤٩)

٢ – فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٞ فَزَادَهُمُ ٱللَّهُ مَرَضٗاۖ (البقرة – ١٠)

٣ – مَثَلُهُمۡ كَمَثَلِ ٱلَّذِي ٱسۡتَوۡقَدَ نَارٗا (البقرة – ١٧)

HUKUMU YA MIM YENYE SUKUN

1. Katika Aya ya kwanza utaona MIM YENYE SUKUN

(وَأَنِ ٱحْكُمْ بَيْنَهُمْ بِمَا)

ipo mahali pawili na zimefuatiwa na herufi ya 'Ba' 'ب' tunasoma

"Wa anih'kum bainahum bimaa"

Kwa hivyo hukumu yake inakuwa 'IKH'FAA PAMOJA NA GHUNNA' na katika kuitamka, inakuwa katika hali baina ya IDH'HAR NA ID'GHAM kama tulivyokwisha eleza nyuma.
Ikiangukia baada ya Mim Yenye Sukun herufi ya 'Ba' nayo ndiyo hiyo hiyo moja tu inakua MIM NI YENYE kufichika pamoja na ghunna. K.m.

وَهُمْ بِالآخِرَةِ – يَعْتَصِمِ بِاللهِ

"Wa hum bil'akhirati"

Mim yenye sukun imefuatiwa na 'b'

Au "Yaatassim billahi"

Mim yenye sukun imefuatiwa na 'b'

Nayo huitwa Ikh'faa itamkwayo midomoni. Kwa Kiarabu inaitwa "IKH'FAAN SHAFAWIYA" إِخفاءً شفويا

2. Katika Aya ya pili utaona MIM YENYE SUKUN imefuatiwa na MIM yenye haraka (tumeeleza kabla kuwa 'haraka' inakusudiwa kuwepo ama fat'ha au kasra au dhamma) kwa Kiarabu huitwa 'MIM MUTAHARIKA' مِيْمٌ مُتَحَرِّكَةٌ kwa hivyo hukumu katika Aya

hii (فِي قلوبهم مِّرَض) ni kuingizwa MIM YENYE SUKUN ya kwanza katika MIM yenye harka ya pili na kutamkwa herufi moja kwa Ghunna: ‘FI QULUBIHIM-MARADHUN’ (TUMETIA MIM MBILI KUONYESHA MKAZO WA MIM).
HUKUMU hii huitwa “ID’GHAM SHAFAWIYYAN AU ID’GHAM MUTAMATHILAYN” (IMEKUWA ID’GHAM KWA KUCHANGANYWA HIZO MIM mbili na kuwa moja na kuitwa SHAFAWIYA kwa sababu unapozitamka unaibana midomo yako pamoja kwa nguvu. Pia huitwa ID’GHAM MUTAMATHILAYN yaani herufi hizo zimefanana (mim na mim ni namna moja) pia herufi nyengine za namna moja ambazo tutajifunza baadaye. Mifano mengine:

Mim mutaharika

لهم مَّا يَشَاؤُونَ – تُنجِيكُم مِّن

Mim yenye sukun

Mim ya kwanza yenye sukun huingizwa katika mim ya pili yenye haraka na kutamkwa kwa hiyo mim ya pili yenye shadda na kutamkwa kwa ghunnah, na unabana midomo kiasi cha haraka mbili (kuhisabu vidole viwili). Huitwa Kiarabu

ادغاماَ شفوياً او إدغام متَماثلين

3. Ama ikiangukia MIM YENYE SUKUN mojapo ya herufi za Alfabeti (isipokuwa herufi mbili BA na MA) inakuwa hukumu yake ni kuwa Mim idhihirike yaani iwe AL IDH’HAAR na unaitamka kutokana na MAKHRAJ yake (kinywani) kwa kuikutanisha midomo miwili pasina ghunnah (yaani kutoa ile sauti kutokea puani) k.m. (مَثَلُهُمْ كمَثَلِ) MATHALUHUM

(جَاءَكُمْ رَسُولٌ – أَنفُسِكُمْ عَزِيزٌ – مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ)

JAAKUM – ANFUSIKUM – ANITUM

Inakuwa Mim inadhihirika kwenye midomo (yaani unaitamka midomoni kwa uwazi) ambayo (katika mafunzo ya kusoma Qur’ani) inaitwa الإِظهـــار الشفوي.

Nayo huwa katika neno moja k.m.

أَنْعَمْتَ – تُمْسُونَ – الأَمْرُ

Mim yenye sukun katika neno moja

Au huwa katika maneno mawili:

(لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ)

Mim yenye sukun imefuatiwa na

(Ta) "ت" katika neno la pili

Tahadhari na kuificha mim (yaani kutoitamka sawa sawa) ikifuatiwa na FA (ف) na WAW (و) kwa sababu hukumu yao kudhihirisha mim (الاظهــار)

Imefuatiwa na FA ( ف ) Mim yenye sukun ( مْ )

لَهُمْ فِي الدُّنْيَا خِزْيٌ وَلَهُمْ فِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ ١١٤ (البقرة)

لَّهُمْ دَرَجَاتٌ عِندَ رَبِّهِمْ وَمَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ٤ (الأنفال)

Imefuatiwa na WAW ( وَ ) Mim yenye sukun ( مْ )

Tutatamka:
Lahum fi-ddunya – Lahum fil'akhirati – Rabbihim wa maghfiratun kwa hivyo Hukumu za Mim yenye sukun ni tatu:

1. Al-IKHFAA
2. AL-ID'GHAM
3. AL-IDH'HAAR

Kwa hivyo zimekusanywa na kusemwa katika beti hii (ili kwa mwanafunzi aweze kuzihifadhi kwa wepesi):

أَحْكَامُهَا ثَلاثَةٌ لِمَنْ ضَبَطَ     إِخْفَاءٌ إِدْغَامٌ وَ إِظْهَارٌ فَقَطْ.

Zimeitwa hukumu za Mim شَفَوِيَّةً kwa sababu ukiitamka inatoka kwenye midomo miwili.

Angalia: Inapasa kudhihirisha ghunnah juu ya Mim ILIYOTIWA SHADDA; kwa mfano ثُمَّ – نِعِمَّاً

## TUJIKUMBUSHE

MIM YENYE SUKUN ina hukumu tatu:

(1) AL-IKH'FAA (yaani unapoitamka herufi baina ya Id'gham na Idh'haar) inapokuwa kwenye 'BA' وَأَمْدَدْنَـٰهُم بِفَـٰكِهَةٍ

(2) AL-ID'GHAM (yaani inapoingizwa herufi ya kwanza katika herufi ya pili na kuwa moja na kutamkwa kwa ghunnah) مَآ أَلَتْنَـٰهُم مِنْ

(3) AL-IDH'HAAR (yaani kuitoa kwenye makhraj (patokeapo herufi) yake bila ya ghunnah) بِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ

## DARSA YA NANE

## المـــد وأقســـامه(١)

### MADDA NA SEHEMU ZAKE

### SEHEMU YA KWANZA

**قال الله تعالى:**

وَيَوْمَ يَعَضُّ ٱلظَّالِمُ عَلَىٰ يَدَيْهِ يَقُولُ
يَٰلَيْتَنِي ٱتَّخَذْتُ مَعَ ٱلرَّسُولِ سَبِيلًا ﴿٢٧﴾ (الفرقان)

MADDA ni kuvuta sauti kwenye herufi katika herufi za Madda tatu. Nazo ni:

(1) ALIF yenye sukun iliyotanguliwa kabla yake na herufi yenye Fat'ha. Kama katika Aya ya Qur'ani hiyo juu neno 'ADHAALIM' 'ظَ' imevutwa na 'alif' 'ظَا' na ina fat'ha; kwa hivyo herufi zinazovutwa na 'alif' daima zinakuwa na fat'ha kiasi cha mvuto huo ni haraka mbili kiasi cha kusema "Moja mbili".

Imevutwa kwa Alif yenye sukun

( الظَّـــا لِمُ )

Dha (ظ) yenye fat'ha

(2) WAW yenye sukun iliyotanguliwa na herufi yenye 'dhamma' katika Aya ya juu kuna maneno mawili nayo ni: YAQOOLU, ARRASOOLU. Qaf na Sin zimevutwa kwa WAW na zina dhamma.

Sin yenye dhamma ( سُ )  Qaf yenye dhamma ( قُ )

( يَقُـــول ، الرَّسُـــول )

Waw zenye sukun

(3) YA yenye sukun imetanguliwa na herufi yenye kasra, katika Aya ni neno moja nalo ni nuni (ن) katika neno 'Yalaytanii'. Nuni inavutwa kwa 'ya'.

( يَا لَيْتَنِي )

Ya yenye sukun

Hizi Madda zimegawanyika sehemu mbili:

(A) Madda ya Asili: Maddil-Asli. أ- أَصلي.

(B) Madda isiyo ya Asili: Maddal-Far'i. ب- فرعي.

Tutaeleza sehemu hizo tukichukua moja moja na aina zake.
Lakini lazima tuelewe kwamba tunatumia majina yake kwa Kiarabu, kwa sababu ni vigumu kutafsiri kwani hayaleti maana ya kufahamika hassa katika Qur'an na kujiepusha kupoteza ilivyokusudiwa katika Qur'an inabidi tujifunze majina kwa Kiarabu na baadaye tutaelewa kwa maelezo na mifano inayotolewa.

(A)Tunaanzia kwa MADDA YA ASILI, nayo kwa Kiarabu:

(أ) المد الأصّلي

Na tutatumia jina hilo AL-Maddal Asli.

Madda hii inaitwa Madda Attabii: (الطَبيْعِيِّ)

Nayo ni Madda ya maumbile iliyokamilika, kwa hivyo haipungui ilivyowekwa wala haizidi kitu juu yake. Na kiasi cha kuvutwa kwake ni haraka mbili (kwa kiasi cha kufunga vidole viwili au kuhesabu moja mbili) Ni Madda ya kawaida ambayo haiwi baada ya herufi yenye Madda ina Hamza au Sukun. K.m.

(a) Qāāla (nimetia āā kuonyesha kuvuta) Alif ina sukun haitamkwi, lakini tunaivuta Qaf kwa sababu imefuatiwa na herufi ya Madda nayo ndiyo hiyo 'Alif'.

قَالَ-

Qaf ina fat'ha na imevutwa kwa Alif

(b) Qaf ikiwa ina dhamma inavutwa kwa herufi ya Madda nayo ni 'WAW'. Tunasoma 'YAQŌOLU'.

يَقُولَ

Qaf ina dhamma inavutwa kwa (Waw)

(c) Qaf ikiwa ina kasra huvutwa kwa 'Ya'. Tunasoma QEELA.

قِيــلَ

Qaf ina kasra inavutwa kwa 'Ya' yenye sukun

## AINA ZA MADDIL-ASLI: من أَنْــوَاعِ المَــدِّ الأَصْلِي:

(1) MADDUL-BADALI: (١) مَدُّ البَدَلِ:

(a) Nayo ni Madda inayokuwa baada ya herufi ya Hamza nayo ni ( أ ) tunapotaka kuivuta kwa alif hatutii hamza ya pili kama hivi ( أ أ )bali tunatia madda ( ~ ) juu ya alif kama hivi: آ ) (kwa mfano neno: ( آمَنَ ) Tunasoma Aamana; tumeongeza a ya pili kuonyesha kuvuta. Kiasi cha kuvuta ni haraka nne na inajuzu kuongeza mpaka haraka tano au sita (Tumesema haraka maana yake kufunga vidole mara nne kwa haraka nne au kuhesabu moja mbili tatu nne).

(b) Tunapovuta herufi ya Hamza kwa Waw. Hamza hii huwa yenye dhamma ( أُ ) k.m. أُوتِينَا– Uutiina.

(c) Alif yenye kasra ( إِ ) huvutwa kwa 'Ya' إِيمَاناً– Iimanan tunatia ii kuonyesha kuvuta.
(Angalia: bora kusoma kwa herufi za Kiarabu kuliko kwa Kiswahili tusije tukasoma sivyo).

(2) MADDU ASSILATI-L-QASEERA: (٢) مَدُّ الــصِلَةِ القَصِــيْرَة:

Nayo ni Madda iliyotakana na 'Ha'. Ha yenyewe ni ya kuonyesha 'kitu chake' k.m. Kitabu chake (mwanamme) Kitabuhu inaitwa 'Ha ya dhamir' yenye kasra au dhamma ikiwa baina ya herufi mbili zenye haraka (tunajua haraka ni fat'ha au dhamma au kasra). K.m.

( قَالَ لَهُ صَاحِبُهُ – إِنَّهُ بِعِبَادِهِ خَبِيرٌ بَصِير)

| | | |
|---|---|---|
| Ha ya dhamir yenye kasra imeangukia baina ya دِ + خَ | Ha ya dhamir yenye dhamma imeangukia baina ya نَ + بِ | Ha ya dhamir yenye dhamma imeangukia baina ya haraka mbili لَ + صَ |

Ama ikiwa kuna herufi yenye sukun kabla ya HA YA DHAMIR au baada yake haivutwi ila katika Qauli ya Mwenyezi-Mungu Mtukufu: ويخلد فيه مهانا

Na huangukia pia hiyo Ha baina ya herufi mbili zenye haraka (yaani ama dhamma ama fat'ha au kasra) wala haivutwi pia k.m. وإِنْ تَشْكُرُوا يَرْضَهُ لَكُمْ:

(3) AL MADDU ATTABIIYYU AL HARFIYYU:

(٣) المَدُّ الطَّبِيْعِيُّ الحَرْفِيُّ:

Nayo ni Madda ya maumbile ya herufi (ndiyo maana ikaitwa ALharfiyyu) nazo ni (ر – هـ – ط – ي – ح) huandikwa pamoja (حي طهر) nazo ni baadhi ya herufi zinazoanziwa baadhi ya Sura.

(Kama zitakapokuja katika darsa ijayo ambazo zinaitwa 'AL AHRUFI ANNURANIYA' (الأَحْرُفِ النُّورَانِيَّةَ)

Kama mfano: (طَاهَا) : (طٰهٰ)

Inasomwa hivi — inaandikwa hivi

(4) MADDUL IWADH: (٤) مَدُّ العِوَض

Madda hiyo ni kusimama kwenye TANWIN (YENYE FAT'HA MBILI ambazo tunaziita Fat'hatein) kwa alif badala ya ile tanwin (yaani tunasimama kwa fat'ha moja na alif mbele yake). k.m. ( سَبِيْلَا ).

Angalia: Aya mwanzo wa darsa utaona imeishia: سَبِيْلاً kwa fat'hatein ndivyo inavyoandikwa. Lakini ukisoma na ukasimama mwisho wa Aya hii unasoma hivyo سَبِيْلَا kwa fat'ha moja na alif imesimama badala ya tanwin (katika kuisoma).

Tukisoma tunaona الطاء inayo herufi mbili 'طَا' Ttaa na tukisoma السين inayo herufi tatu سين (١ ٢ ٣) Sin, pia tukisoma الميم inayo herufi tatu ميم (١ ٢ ٣) Mim. Herufi ya katikati ndiyo herufi ya Madda.

## (5) MADDU ATTAMKIN: (٥) مَدُّ التَّمكِيْنُ:

MADDU ATTAMKIN ni 'YA' YA MADDA inapoangukia kabla ya YA MUTAHARRIKA. Kwa mfano:

(الذِي يُوعَدُون)

'YA' MUTAHARRIKA — 'YA' YA MADDA

Pia WAW YA MADDA inapoangukia kabla ya WAW MUTAHARRIKA k.m.

(آمنُوا وَعَمِلُوا الصالِحَاتِ)

'WAW' MUTAHARRIKA — 'WAW' YA MADDA

Pia YA YENYE MADDA inapoangukia baada ya YA yenye shadda k.m.

( حُيِّيتُمْ )

'YA' YA MADDA — 'YA' YENYE SHADDA

## TUJIKUMBUSHE

(1) Herufi za Madda ni tatu:
- (i) 'ALIF' YENYE SUKUN inapokuja herufi yenye fat'ha
- (ii) 'WAW' YENYE SUKUN inapokuja kabla yake herufi yenye dhamma
- (iii) 'YA' YENYE SUKUN inapokuja herufi yenye kasra kabla yake

(2) MADDA imegawika sehemu mbili:
- (i) ASLI
- (ii) FAR'I

(3) SEHEMU ZA MADDIL-ASLI ni 5:
- (i) MADDAL- BADAL
- (ii) MADDAL- ASSILAT AL QASEERA
- (iii) MADDAL- IWADH
- (iv) MADDAL- ATTABIYYU AL HARFIYYU
- (v) MADDAL- ATTAMKIN

DARSA YA TISA

# المــد وأقسـامه(٣)

**قال الله تعالى:**

وَالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِمَآ أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَآ أُنزِلَ مِن قَبْلِكَ
وَبِالْآخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ ﴿٤﴾ أُولَٰٓئِكَ عَلَىٰ هُدًى مِّن
رَّبِّهِمْ ۖ وَأُولَٰٓئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٥﴾ (البقرة)

## MADDA NA SEHEMU ZAKE
## SEHEMU YA PILI (2)

Tunaona katika Misahafu mitukufu alama hii (~) juu ya herufi za Madda kwa mfano (بِمَـآ أُنزِلَ – وَمَـآ أُنزِلَ – أُولَـٰٓئِكَ). Hii inaonyesha kuwa herufi za Madda katika mifano hii inatakikana tuzivute zaidi kuliko zile za Attabiiyyu tulizokwisha kuzisoma. Tukichungua HERUFI ambayo inayofuata Madda, tunaona ni HAMZA.

Madda hii ni ile ya sehemu ya pili inayoitwa AL MADDUL–ALFAR'I. Madda Al-Far'i imezidi katika kuvutwa kwake kwanza kwa sababu ya Hamza; pili kwa sababu ya Sukun, kwa hivyo kuvutwa kwake kunazidi haraka mbili.

Maddul Far'i imegawika sehemu mbili:-

(1) Al Maddul wajib Al Muttasil: (١) المَدُّ الوَاجِبُ المُتَصِلِ:

Imeitwa WAJIB kwa sababu tunaposoma inatulazimu kuivuta zaidi kuliko ile ya Attabiiyyu na imeitwa MUTTASILAN kwa sababu Madda na Hamza zimeshikamana katika neno moja, na kuvutwa kwake kunakisiwa kiasi cha haraka nne au tano, wengi wanapendelea haraka nne. k.m.

(أُلَـٰٓئِكَ) – (سِيِّئَـٰتُ) – (الملَـٰٓئِكَةُ) – (تَبُـوٓءَ)

Madda na Hamza
katika neno moja

## (2) AL MADDUL JA'IZU AL MUNFASILU: (٢) المدّ الجائز المنفصل:

Madda hii imeitwa JAIZAN kwa kuwepo hitilafu katika usomaji, baadhi ya Wataalamu wa Tajweed wanasema inavutwa zaidi, wengine wanafupisha, wengine wanasema inafaa yote mawili. Na imeitwa 'Munfasilan' kwasababu Madda imo katika neno moja na Hamza ipo katika neno la pili. (Yaani munfasil, imefasiliwa au imewekwa mbali na muttasil maana yake imeunganika katika neno au kitu kimoja) kiasi cha kuvuta kwake ni 'haraka' nne mpaka tano ikiwa tumeyasoma yote maneno mawili, la tukisimama mwisho wa neno la kwanza itakuwa Madda Tabii na mvuto wake kiasi cha haraka mbili. Mifano ya Maddul Jaiz Al Munfasil:

Madda katika neno la kwanza

(بمَـــآ أُنْزِلَ – قُوآ أَنْفُسَكُمْ – إِنّيِ أَمَنْتُ)

Hamza katika neno la pili

Na katika Maddul Jaizul Munfasil, kuna Madda Silatel Attawila. Nayo Madda iliyotokana na 'Ha' ya Dhamir yenye kuonyesha kitu chake mwanamme (kama tulivyokwishataja nyuma Madda Assilat Al-Qaseera) inakuwa yenye kasra na kuvutwa na 'ya' ndogo au ina dhamma na kuvutwa na waw ndogo nayo hiyo 'Ha' huangukia baina ya herufi mbili zenye haraka ama kasra ama dhamma, ambapo hiyo herufi ya pili ina hamza. K.m.

Hamza




Waw ndogo na juu yake Madda na imefuatiwa na Hamza

'Ha' ya dhamir

Imeitwa 'Attawila' kwa sababu imevutwa na 'Waw ndogo' na juu yake 'madda' kwa hivyo uvutaji wake unakuwa zaidi kuliko Madda Assilat Al Qaseera ambayo ipo waw ndogo tu kama hapo juu 'Lahu' imetiwa mbele yake waw ndogo tupu.

Mifano mengine:



'Ya' ndogo ya Madda juu yake na imefuatiwa na Hamza

'Ha' ya dhamir yenye kasra

## TUJIKUMBUSHE

AL MADDU AL FAR'IYYU ni yenye kuzidi kuvutwa kwake zaidi ya haraka mbili na inakuwa hivyo kwa sababu ya HAMZA au SUKUN.

Madda inayosabibisha na Hamza ni aina mbili:

(1) AL MADDUL WAJIB AL MUTTASIL na inakua Madda na Hamza katika neno moja.

(2) AL MADDUL JAIZU AL MUNFASIL inakuwa Madda katika neno moja na Hamza katika neno la pili kwa hivyo yanakuwa maneno mawili yaliyofasiliwa mbali mbali. Kiasi cha kuvuta zote aina mbili ni haraka nne mpaka tano lakini inayochaguliwa zaidi katika Madda hizi 2 ni haraka nne.

(3) Pia inatokana na Maddul - Jaizu - Munfasilu, Maddu Assilat Attaweela. Nayo 'Ha' ya (dhamir) yenye kuonyesha kitu chake mwanamme, imeitwa Attaweela kwa sababu 'Waw' au 'Ya' ndogo inayosababisha kuivuta hiyo 'Ha' inakuwa na Madda juu yake na inavutwa zaidi kuliko Maddu-Assilat-al-Qaseera. 'Ha' hii inakuwa ama ina dhamma au kasra na inaangukia baina ya haraka mbili inayofuatwa na Hamza.

DARSA YA KUMI

# المــد وأقســامه (٣)

قال الله تعالى:

أَلَمْ يَجِدْكَ يَتِيمًا فَآوَىٰ ﴿٦﴾ وَوَجَدَكَ ضَالًّا
فَهَدَىٰ ﴿٧﴾ وَوَجَدَكَ عَائِلًا فَأَغْنَىٰ ﴿٨﴾ (الضحى)
الٓمٓ ﴿١﴾ تَنزِيلُ الْكِتَابِ لَا رَيْبَ فِيهِ مِن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٢﴾ (السجدة)

## MADDA NA SEHEMU ZAKE
## SEHEMU YA TATU (3)

Imetupitia katika darsa iliyopita kwamba MADDA AL FAR'I inakuwa kwa sababu ya HAMZA NA SUKUN na tumejifunza sehemu ya kwanza (nayo ni kuwa Madda Alfar'i inayosabibishwa na Hamza). Na katika darsa hii tunajifunza MADDA Al FAR'I inayosabibishwa na SUKUN. Ikiwa baada ya Herufi yenye Madda, herufi yenye sukun (pamoja na kuzingatia kwamba herufi yenye shadda ni mfano wa herufi mbili ya kwanza ina sukun na ya pili ina haraka k.m. الجَنَّة tukiisoma 'AL-JANNAH').

Madda inayosabibishwa na Sukun imegawika sehemu mbili:-

(1) AL MADDUL ALLAZIM. (١) المَدُّ الَّلازِم.

(2) AL MADDUL AL-ARIDH. (٢) المَدُّ العَارِض.

Tukianzia (1) AL MADDUL ALLAZIM: (١) المَدُّ الَّلازِم:

Nayo huwepo baada ya herufi ya Madda, herufi yenye sukun ambayo sukun hii ni ya asili na kiasi cha kuvuta kwake ni haraka sita pasina kuzidi wala kupungua! Na Madda hii ya ALLAZIM inagawanyika sehemu nne:

(a) AL MADDU ALLAZIM AL MUTHAQQAL ALKALIMI:

( أ ) المَدُّ الَّلازِمُ المُثَقَّل الكَلميِّ:

Imeitwa LAZIMAN kwa kulazimika kuwa na SUKUN juu ya herufi inayokuwa baada ya herufi ya Madda tunapo sita kusoma au tunapoendelea. Na imeitwa MUTHAQALLAN kwa kuwepo SHADDA juu ya herufi inayokuja baada ya herufi yenye MADDA. Na inaitwa KALMIYYAN kwa sababu inakuwa katika

maneno ya Qur'an Tukufu tu kama maneno yafuatayo:

Herufi yenye shadda baada ya herufi yenye Madda

(وَلاَ ٱلضَّـــآلِّينَ – ٱلْحــآقَّةُ– الصـَّــآخَّةُ)

Herufi yenye Madda ina sukun

Tunaivuta 'Dhad-ض' haraka sita, imesababishwa kuvutwa hivyo kwa sababu ya kuwepo herufi yenye Madda mbele yake na ina alama ya Madda ( آ ) juu yake. Herufi iliyofuatia ni Lam yenye shadda tunaik̂aza hivi lli na imefuatiwa na herufi ya Madda Attab̂iīyyi tunaivuta Ilii haraka mbili. Tunasoma:

SHADDA KWENYE LAM

1 2 3 4 5 6 -<س>-12

WALADHAAAAAALLIIN

Haraka 6 Haraka 2

Tunasoma:

SHADDA

1 2 3 4 5 6- س -
1 2

AL - HAAAAAAQQATU

Haraka 6

SHADDA

1 2 3 4 5 6 - س -

ASSAAAAAA KHKH ATU

Haraka 6

(b)AL MADDU ALLAZIM AL MUKHAFIF AL KALIMY:

(ب) المَدُّ الَّلازِم المخفف الكلمي:

Imeitwa MUKHAFFAFAN kwa sababu herufi inayoangukia baada ya herufi yenye Madda ni yenye sukun pasina Id'gham kwenye herufi yenye Madda; wala hamna shadda

matamshi yake ni khafifu hatukazi. Na hakuna katika Qur'an yote ila neno moja tu katika Surat Yunus limekaririwa mara mbili nalo ni آلآنْ.

(c)AL MADDUL ALLAZIM AL MUTHAQAL AL HARFY:

(ج) المَدُّ اللَّازِمِ المثقل الحرفي:

Imeitwa 'HARFIYAN' kwasababu inakuwa katika herufi ziliopo mwanzo wa Sura

1 2 3 4 5 6

k.m Alif – Laaaaaa – Miim (أَلِفْ لاَمْ مِّيم).

(d) AL MADDUL ALLAZIM AL MUKHAFAF AL HARFY:

(د) المَدُّ اللَّازِمِ المخفف الحرفي:

Nayo ni khafifu kwa sababu herufi inayofuatia herufi yenye madda haziingiani yaani hamna id'gham.

HERUFI ZENYEWE NI: (قٓ – نٓ – صٓ).

2- AL MADDUL-ARIDH LI-SUKUN: (٢) – المَدُّ العَارِضُ لِلسُّكُون :

Neno 'Aridh' ni kizuwizi au pingamizi yaani yenye kuzuia au kupinga kwa hivyo Madda hii inaangukia baada ya herufi yenye Madda yenye sukun, yenye kusabibisha kusimama unaposoma Qur'an. Huko kusimama ndiko kulikokusudiwa kizuizi ikaitwa Maddul-Aridh; unasimama ama mwisho wa Aya au penye alama ya kusimama na neno hilo hutamkwa kwa sukun.

Al – kitab, lilmuttaqin n.k (الكِتَابْ – لِلمُتَّقِينْ – يَعْقِلُونْ)

Haiandikwi sukun hiyo bali inatamkwa unaposimama mwisho wa Aya na kadhalika.

Inakutana na Maddul-Aridh-Lissukun, Madda nyengine inayoitwa Maddul-Llyn مَدُّ اللِّين nayo ni Waw na Ya huwa zote mbili zina sukun na herufi iliyopo kabla ya (herufi hizo zenye sukun) huwa zenye fat'ha na unasimama katika kusoma k.m. Quraysh – Khawf.

(قُرَيْشْ – خَوْفْ)

Maddul-Aridh
Shin ina Sukun ukisimama

Maddul-Llyn
Ya ina sukun

Ra ina fatha

Kiasi cha kuvuta Maddul-Aridh na Maddu-Llyn ni haraka mbili au haraka nne au sita unaposimama. Ama unapoendelea kusoma

unavuta Maddul-Aridh haraka mbili ikiwa herufi ya mwisho haina hamza na unavuta haraka nne au tano ikiwa herufi ina Hamza kama 'yashaaa' (يَشَاءُ) ingawa inaandikwa dhamma mwisho 'yashaau' lakini tukisita ina sukun katika kutamka (يَشَاءْ) kwa sababu hiyo ni 'Wajib Muttasil'. Ama Maddu-Llyn haivutwi kabisa ukiendelea kusoma.

## TUJIKUMBUSHE

Zinagawika Madda zinazosababishwa na sukun sehemu mbili:

(1) Lazim (المد اللازم)

(2) Aridh (المد العارض)

(1) Tukianza sehemu ya kwanza nayo ni Al - Madda Allazim imegawika sehemu nne.

(a) Al-Maddu Allazim Al-Muthaqal Al-Kalimy

Huwepo baada ya herufi yenye Madda, herufi yenye shadda. (Tulisema kwamba herufi yenye shadda asili yake herufi mbili ya kwanza ina sukun na ya pili ina haraka k.m:

الصَّـــآخَّةُ - الضَّـــآلِّين

Tunasoma hivi: الصْصَاخْخَةَ - الضْضَالْلِيْن

(b) Al-Maddu Allazim Al-Mukhafaf Al-Kalimy au Al-Maddu Allazim Al-Kalimy Al-Mukhafaf (zote sawasawa).

Imeitwa Mukhafaf kwa sababu herufi baada ya herufi ya Madda ina sukun, pia hamna Id'gham wala shadda.

Ni neno moja tu katika Qur'an lililo kaririwa mara mbili katika Surat Yunus neno ni آلآنَ

(c) Al-Maddu Allazim Al-Mthaqal Al-Harfy

Imeitwa "Harfiyan" kwa sababu inakuwa katika herufi ya Hijaiya ziliopo mwanzo wa Sura k.m. الف لام را (الر)

n.k.

(d) Al-Maddu Allazim Al-Mukhafaf Al-Harfy
Imeitwa Mukhafaf kwa sababu herufi inayofuata herufi ya Madda si mudghama (yaani hamna Id’gham) k.m.

قٓ – نٓ – صٓ

Ukisoma ni herufi tatu ق + ا + ف

ya kati ndiyo ya Madda (**الف**) na (**ف**) ni mudghama n.k.

(2) Sehemu ya pili ya Madda inayosabibishwa na sukun ni <u>AL MADDU AL ARIDH</u>.

Inakua sukun yake Aridhan (kama tulivyosema Aridh ni kizuizi na hapa imekusudiwa kusimama mwisho wa Aya au mahali palipotiwa alama ya kusimama; na unasimamia kwa sukun. k.m. **الرحمٰنْ – للمتقينْ – يعقلونْ**

Mfano wa Maddel Aridh Lissukun ni Maddel Llyn **مد اللين**

Nayo ni ‘WAW’ na ‘YA’ zilizotiwa sukun na herufi iliyo kabla yao imetiwa fat’ha na kusimama kwenye herufi zilizo baada yake kwa sukun. na kuvuta kwa zote mbili; Maddel-Aridh na Allyn ama haraka mbili, au nne au sita unaposimama. K.m.

**البَـيْـتْ**

herufi unayosimamia baada yake ina sukun

herufi kabla yake ina fat'ha

Maddel-Llyn

Vile vile **الصَّيْـفْ**

# المـد وأقسـامه

المد اطالة الصوت بحرف من حروف المد وهى أ . و . ى – مجموعة فى (نوحيها)

- أصلي (طبيعي) وهو الذي لا تقوم ذات الحرف الا به ولا يتوقف على سبب من همز أو سكون ( قال – يقول – قيل) يمد على حركتين
  - ويلحق به
    - البدل: مد الحرف المبدل عن همز ساكن بعد همز (أمن – إيماناً – أوتىِ)
    - العوض: الوقف بالألف على تنوين النصب (كتاباً)
    - الصلة الصغرى: الهاء بين متحركين (ماله يتزكى)
    - الطبيعي الحرفي: حروف (حى طهر) ح . ي . ط . ه . ر (طه)
    - التمكين: ياءان أولاهما مشددة (حييتم)
- فرعى: ما كان بسبب الهمز أو السكون
  - بسبب الهمز (٤-٥ حركات)
    - واجب متصل: حرف المد والهمزة بكلمة واحدة جاء- جئ- سوء
    - جائز منفصل: حرف المد في أخر كلمة والهمزة في أول كلمة ثانية (يا أيها- توبوا إلى الله- الذي أخرج) ويلحق به مد الصلة الكبرى (لم يره أحد) (الهاء بين متحركين الثاني همز)
  - بسبب السكون
    - السكون عارض (٢-٤-٦ حركات) (عرض بسبب الوقف) (رجيمْ- نستعينْ- يعلمونْ) ويلحق به مد اللين (قريْش- بيْت- خوْف)
    - السكون أصلي (٦ حركات لازم)
      - حرفي
        - مثقل: بعد حرف المد شدة (الم) لا ميم
        - مخفف: بعد حرف المد سكون (ن) نون
      - كلمي
        - مثقل: بعد المد شدة (اطامّة)
        - مخفف: بعد حرف المد سكون (آلآن)

DARSA YA KUMI NA MOJA

# مخارج الحروف(١)

**قال الله تعالى:**

وَمَن يَبْتَغِ غَيْرَ ٱلْإِسْلَٰمِ دِينًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِى
ٱلْـَٔاخِرَةِ مِنَ ٱلْخَٰسِرِينَ ﴿٨٥﴾ (آل عمران - ٨٥)

ٱلْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِى
وَرَضِيتُ لَكُمُ ٱلْإِسْلَٰمَ دِينًا ( المائدة - ٣ )

## ZINAKOTOKEA HERUFI – SEHEMU YA KWANZA

Tutatumia neno la Kiarabu ‘Makh’raj’ yaani panapotokea herufi za Kiarabu katika kinywa ikiwa mahali pengi husemwa ‘Makhaarij’ ili tulete maana kamili ya mahali pasina kufasiri ambako inabidi kutumia maneno mengi hata ifahamike maana iliyokusudiwa.

Tukitaka kusoma Qur’ani kwa matamshi mazuri yapasayo kutamkwa (yaani ni lazima kutamka sawa) hatuna budi na kuzitoa kila herufi kwenye makh’raj yake! Tukikosea tunaingia makosani! Inabidi tujikaze kuzitoa kwa Kiarabu kwa mfano: Qaf (ق) sio Kaf (ك) – Hha (ح) sio ha (ه) na kadhalika.

Namna ya kujua wapi makh’raj ya herufi (baada ya kwisha kujifunza matamshi ya herufi zote kwa Kiarabu) ni:-

(a) Tutie sukun herufi yenyewe au

(b) Tuitie shadda na tuikaze tunapoitamka baada ya HAMZATEL-WASL (tutaeleza baadaye) na inakoishia sauti ndiko makh’raj yake. Kwa mfano tuchukue herufi ya Mim (م) tunasema (kwa sukun) (امْ) au kwa shadda (امَّ) (unaitamka Am au Amma) utaona inaishia kwenye midomo kwa hivyo tunasema Makh’raj yake kwenye midomo kwa Kiarabu tunaita ‘Shafawiyun’ شَفَوِيٌ na kadhalika. Tuliwahi kuzitaja makhaarij kubwa yaani kwa Kiarabu zinaitwa:

## مَخَارِجُ رَئِسِيَّةَ

Zimegaiwa hizi Makhaarij kuu katika sehemu tano na katika hizo kuu zimo makhaarij kumi na saba (17) zilizochambuliwa moja moja. Makhaarij kuu (yaani kubwa kabisa) ni:-

المَخَارِجُ الرَّئِيْسِيَّةُ فَهِيَ: الجَوْفُ –الحَلْقُ –اللِّسَانُ –الشَّفَتَانِ –الخَيْشُومُ.

Makhaarij kuu ni:-

(1) Uwazi wa ndani baina ya koo na kinywa
(2) Koo
(3) Ulimi
(4) Midomo miwili
(5) Sehemu ya puani (au sauti ya kipuani).

1- Uwazi wa ndani baina ya kinywa na koo, unaitwa AL-Jawf: (١) الجَوْفُ

Katika makh'raj hiyo zinatoka herufi tatu:
(a)Alif yenye sukun iliyotanguliwa na herufi yenye Fat'ha
(b)Waw yenye sukun iliyotanguliwa na herufi yenye Dhamma
(c)Ya yenye sukun iliyotanguliwa na herufi yenye Kasra

Nazo ni herufi za Madda na zinaitwa pia herufi za uwazi wa ndani baina ya kinywa na koo حُرُوفُ الجَوْفِ au الحُرُوف الْهوائيةَ.

Au Huruful-Hawaiya kwa sababu zinatoka kwenye hewa iliyopo katika uwazi wa ndani baina ya kinywa na koo.

2- Koo: Nayo inaitwa kwa Kiarabu AL Hhalq ( ٢ ) الحَلْقُ:

Ndani ya koo zimo makhaarij tatu kwa herufi sita:
(a) Koo ya ndani kabisa inayofuatia kifua nayo inaitwa:

أ – أَقْصَى الحَلّق

Inayo herufi mbili Hamza na Ha. الهـــاء و الهمزة

( هـ ) و ( أ )

(b) Sehemu ya katikati ya koo inaitwa: (ب) وَسَطَ الحَلْق:

Zinatoka humo herufi mbili Ayn na Hha (العين والحاء) (ع وح)

(c) Sehemu ya juu ya koo inayoelekea kinywa inaitwa:

(ج) أدنى الحَلْق:

Zinatoka herufi mbili Ghein na Kha (الغين و الخاء) (غ و خ).

Na hizi herufi sita ni zile zile herufi za IDH'HAAR zinazotoka kooni (tulizokwisha kujifunza) na zinaitwa HERUFI ZA KOONI kwa Kiarabu الحُرُوف الحَلْقِية.

## TUJIKUMBUSHE

Makhaarij kuu za herufi ni tano (5) nazo:

(1) Uwazi wa ndani wa koo الجوف.

(2) Koo: Nayo ina Makhaarij tatu kwa herufi sita,

(a) Koo ya ndani kabisa inayoishia kifuani: أ - أَقصى الحَلَق

Zinatoka herufi mbili الهمزة والهــاءُ.

(b) Sehemu ya katikati ya koo ب - وَسَط الحلْق

Zinatoka herufi mbili Ayn na Hhaa العينُ والحاءُ.

(c) Sehemu ya juu ya koo kuendea kinywani ج - أَدنى الحلق

Zinatoka herufi mbili pia الغينُ والخاءُ.

DARSA YA KUMI NA MBILI

# مخارج الحروف(٢)

قال الله تعالى:

وَقُلْ جَآءَ ٱلْحَقُّ وَزَهَقَ ٱلْبَٰطِلُ ۚ إِنَّ ٱلْبَٰطِلَ كَانَ زَهُوقًا ﴿٨١﴾
(الإسراء)

## MAKHAARIJ YA HERUFI – SEHEMU YA PILI (2)

Tunaendelea na Makhaarij zilizobakia ambazo zilizo kuu. Ya tatu:

3- ULIMI: (٣) اللســـان

Una makhaarij kumi na herufi kumi na nane:

(a)Sehemu ya ndani kabisa ambayo hufuatiwa na koo ( أ ) أَقصى اللسان.

pamoja na sehemu iliyokabili sehemu ya juu ndiko inakotokea herufi ya Qaf (القـــاف).

(b)Chini kidogo ya makh'raj ya Qaf (ب) أقصى اللســـان.

inatoka herufi ya Kaf (الكـــاف). Herufi mbili hizo zinaitwa 'Lahawiyan' (لَهَوِياً) kwa kunasibiana na kilimi mwisho wa ulimi kinaitwa (Allahati) اللَّهــــاةِ.

(c)Sehemu ya katikati ya ulimi: (ج) وسط اللســـان:

Ni sehemu iliyoelekeana na sehemu ya juu ya kinywa.

Na zinatoka herufi: وَالحُرُوفُ (الجِيمُ وَالشِّيْنُ وَاليَاءُ غيرُ المدّيّة)

Jim na Shin na Ya; lakini sio Ya ya Madda. Zinaitwa herufi hizi Herufi Ashajriya

(الحروف الشَّجَرِيَّة)

yaani za katikati ya ulimi inaitwa Shajril-Lisan.

شجْرِ اللســـان أَي وسطِه

(d)Kutokana na moja ya pembe za: (د) مِنْ إِحْدَى حَافَتَي اللِّسَان:

ulimi (Kulia na kushoto) na sehemu inayokabiliana na magego ya juu inatoka humo herufi ya Dh-dhad (الضـــاد).

Herufi hii ya Dh-dhad inawashinda watu wengi kuitamka hata Warabu wenyewe kwa hivyo inabidi tufanye mazoezi sana hata tuweze kuitamka vilivyo, tuwe na hadhari sana tusiitamke kama dha (ظ).

(e)Baina ya pembe mbili za ulimi - :مَا بَينَ حَافَتَي اللِّسَان مَعاً (هـ) pamoja na baada ya Makh'raj ya Dh-dhad na sehemu inayokabiliana na ufizi wa juu inatoka herufi ya Lam (اللَّامُ). Makh'raj ya 'Lam' ni yenye wasaa zaidi (yaani kubwa zaidi kuliko makh'raj ya herufi zote).

(f) Sehemu iliyo baina ya ncha ya ulimi :مَا بَيْنَ رَأْسِ اللِّسَانِ (و) (au kichwa cha ulimi kwa Kiarabu) na sehemu iliyokabiliana na ufizi wa meno mawili ya mbele ya juu inatoka herufi ya Nuni (النُونِ).

(g)Sehemu iliyopo baina ya ncha ya ulimi:مَا بَيْنَ رَأْسِ اللِّسَانِ (ز) na mgongo wake inayofuata ncha ya ulimi na sehemu iliyokabiliana na ufizi wa meno mawili ya mbele ya juu inatoka herufi ya Ra (ر).

(h)Sehemu iliyopo baina ya mgongo: مَا بَيْنَ ظَهْرِ رَأْسِ اللِّسَانِ (ح) wa ncha ya ulimi na mwanzo wa meno mawili ya mbele ya juu zinatoka herufi za Tt-a – Ta – Dal

(الدَّالُ– التَّــاءُ – الطَّاءُ)

Nazo zinaitwa Herufi Annatt'iiyah (الحُرُوفُ النَّطْعِيَّةُ) yaani herufi za sehemu ya juu ya mbele ya kinywa.

(i) Herufi zitokazo kwenye ncha ya ulimi. :مِنْ رَأْسِ اللِّسَانِ (ط)

Nazo huitwa herufi zenye sauti ya kifirimbi (حُرُوفُ الصَّفِيْرِ). Nazo ni herufi ya Ssad na Zay na Seen

(السِّيْنُ و الزَّاي و الصَّادُ)

(j) Kutokana baina ya ncha ya ulimi na :مِن بَيْنِ رَأْسِ اللِّسَانِ (ي) ncha za meno mawili ya mbele ya juu zinatoka herufi za Dhal, Tha, Dha-ظ (الذَال – والثَّـــاء – والظَّـــاء) na zinaitwa herufi za ufizi (الحُرُوفُ اللَّثَوِيَّة).

4- Makh'raj kuu ya nne baada ya Ulimi ni MIDOMO MIWILI:

(٤) الشَّفَتـــان:

Nayo ina makhaarij mbili mbali mbali nazo:

(a) Sehemu ya undani wa mdomo wa :أ- بطن الشفة السفلى chini na ncha za meno mawili ya mbele ya juu inatoka 'FA'. (الفاء)

(b) Herufi baina ya midomo miwili :ب- من بين الشفتين

uifungapo zinatoka herufi za MIM NA BA الميم و البـــاء Na unapofunga midomo inatoka 'WAW' Lakini sio ile Waw ya Madda (inayotumika kuvutia herufi) الوَاوُ غَيْرُ المَدّيَّة.


5- Sehemu kuu ya tano ni 'KHAYSHUM' ٥- الخَيْشُومُ: وَهُوَ الأَنْفُ maana yake ni pua. Na zinatoka humu herufi za Ghunna

أَحْرُفُ الغُنَّة

Nazo ni Nuni na Mim zenye shadda na Nuni yenye sukun na Tanween, zinapokuwa hizo tanween zimeingia katika herufi zifuatazo (و – م – ن – ي) yaani Id'gham na katika hali ya kugeuzwa (IQLAAB) Nuni kuwa Mim inapokutana na Ba na inapokuwa na herufi za Ikh'faa na Mim yenye sukun inapoingiliana na Mim (nyengine) yaani Id'gham na inapofichika inapokuwa na Ba.

(Angalia darsa za Id'gham, na Ikh'faa na Iqlaab).

Ramani ifuatayo ya kuonyesha sehemu zote za Makhaarij ya herufi na majina yake kwa Kiarabu.




MAKHAARIJ YA HERUFI

Tukianzia kwa mujibu wa Nambari zilizotiwa kwenye diagram ya juu:

(1) Herufi za shafawiya: (Midomo) ni

(a) Undani wa mdomo wa juu na ncha za meno ya juu inatoka ‘Fa’.

(b) Midomo miwili zinatoka Ba – Mim – Waw (siyo ya Madda.

(2) Herufi za Allathawiya: Kutoka ncha ya ulimi na ncha za meno ya mbele ya juu mawili zinatoka herufi:

(Dha – Dhal – Tha) **(ظ- ذ- ث)**.

(3)Herufi mbili za ncha ya ulimi (Lam – Nuni) ن - ل.

(4)Herufi za Annatt-iyah: kutoka kwenye sakafu ya juu ya kinywa na meno mawili ya mbele ya juu zinatoka herufi (TTa – Dal – Ta) (ت - د - ط) .

(5)Herufi za Al Asaliya: zinatoka herufi za Assafir (kama kifirimbi) zinatoka: (Ssad – Za – Sin) (س - ز - ص).

(6)Herufi za Ash-shajriya: zinatoka kati ya ulimi nazo ni (Jim – Shin – Ya) isiyokuwa Ya ya Madda (ي- ش - ج) .

(7)Al – Harfani Allahwiyan (Herufi mbili zitokazo kwenye kilimi mwisho wa ulimi), nazo ni Qaf na Kaf (ك - ق).

(8)Al Huruful – Halqiyah – Herufi za koo, nazo zile herufi sita tulizokwisha kujifunza nazo ni: Hamza – Ha – Ayn – Hha – Ghayn na Kha (خ - غ - ح - ع - هـ - أ).

(9)Al – Huruful – Jawfiyah: Zitokazo ndani ya koo na kinywa katika uwazi ndani ya koo na kinywa na zinatoka herufi za Madda tatu ‘Alif’ na ‘Wa’ na ‘Ya’.

## TUJIKUMBUSHE

Ingawa Makhaarij za herufi na majina yake yanaonyesha ugumu wa kufahamu lakini tusisahau kwamba herufi hizo nyingi tunazijua na tunazitamka vyema zile zilizomo katika Alphabeti ya Kiswahili. Zile ambazo hazimo ndizo za kuchukua jitihada kujifunza kuzitamka vilivyo. Ni vizuri tukijua majina yao yote kwa Kiarabu. Herufi zenyewe ni chache kabisa: ق ،ع ،ط ،ض ،ص

DARSA YA KUMI NA TATU

# صفات الحروف (١)

**قال الله تعالى:**

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾ (القلم)

لَقَدْ جَآءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُم بِٱلْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢٨﴾ (التوبة)

## SIFA ZA HERUFI (1)

Kama ilvyo kila herufi ina Makh'raj yake, hivyo hivyo kila herufi ina namna yake ya kuonyesha kupambanuka kwake (na herufi nyengine) katika Makh'raj yake; na kwa hivyo namna yenyewe ndio sifa yake. Sifa zinagawika sehemu mbili:

(1) Sifa zenye kinyume chake au dhidi yake: (١) صِفَاتٌ مُتَضَادَّة zinaitwa 'Mutadhaaddah'.

(2) Sifa zisizo na kinyume chake au (٢) وصِفَاتٌ غَيْر مُتَضَادَّة dhidi yake zinaitwa 'Sifaatun ghayr Mutadhaaddah'.

Tukianzia Sifa zenye kinyume chake **الصفاتِ المتضادّة** idadi yake ni sifa kumi na hapana budi kwa kila herufi isifike sifa tano katika hizo:

SIFA ZENYE KINYUME CHAKE: 10

1. AL HAMS: ١ – الهَمْسُ

Maana yake kilugha ni Kuficha, lakini katika Qur'ani ni kutoka pumzi (au upepo) wakati unapoitamka herufi kwa sababu ya udhaifu wa kutegemea kwake (hiyo herufi) kwenye Makh'raj yake. Herufi zake ni kumi. Nazo ni:

ف – ح – ث – هـ – ش – خ – ص – س – ك – ت

Wataalamu wameziweka katika maneno haya:-

(فحثّه شخصٌ سكَت)

ili wepesi kuzihifadhi kwa moyo.

## 2. AL JAHR — ٢ – الجَهْرُ

Maana yake kilugha ni kutangaza (kudhihirisha) lakini katika Qur'ani; kuzuia pumzi unapotamka herufi kwa sababu ya nguvu ya kutegemea kwake kwenye Makh'raj. Al – Jahr ni kinyume cha Al – Hams na herufi zake ni zile zisizotajwa katika Al Hams.

## 3. ASH-SHIDDAH — ٣ – الشِدَّةُ

Kilugha maana yake 'Nguvu' ama katika Qur'an ni kuzuilika sauti unapotamka herufi kwa ajili ya kukamilika kutegemea kwake kwenye Makh'raj na herufi zake ni nane zinazowekwa pamoja na kusemwa (أَجَدْ قَطٍ بَكَتْ) Nazo ni:

أ– ج– د– ق– ط– ب– ك– ت

Na vile vile zipo herufi zilizo kati kwa kati baina ya Ash-shiddah na Arrakhawah nazo ni 5: ل– ن– ع– م– ر Wataalamu wameziweka pamoja (لِنْ عُمَرُ).

## 4. ARRAKHAWAH — ٤ – الرَّخَاوَةُ

Kilugha ni ulaini, katika Qur'ani kupita sauti pamoja na herufi kwa ajili ya udhaifu wa kutegemea kwake katika Makh'raj. Herufi zake ni zile zisizokuwa katika Ash-shiddah wala zile za kati kwa kati.

## 5. AL – ISTIILAA — ٥ – الاسْتِعْلاَءُ

Kilugha ni mnyanyuko, katika Qur'ani ni kunyanyuka ulimi unapoitamka herufi na hugusa sehemu ya juu ya kinywa inayoitwa Al hank – al – aala الحَنْكِ الأَعْلَى na herufi zake ni nane nazo ni: خ– ص– ض– غ– ط– ق– ظ Zimewekwa pamoja na kusomwa (خُصَّ ضَغْطٍ قِظْ).

## 6. AL – ISTIFA'L — ٦ – الإِسْتِفَالُ

Kilugha maana yake: Kuteremka (kuwa chini). Ama katika mafunzo ya Qur'ani ni kuulaza ulimi inapotoka herufi kutoka sehemu ya juu mpaka sehemu ya chini ya kinywa na herufi zake ni zile zisizokuwa za Al – Istiilaa.

7. AL – ITTBA'Q — ٧ – الإِطْبَاقُ

Kilugha ni kuganda ama katika Qur'ani ni kugusa ulimi kwenye sehemu ya sakafu ya juu ya kinywa unapotamka herufi, na herufi zake ni nne: (ص – ض – ط – ظ).

8. AL – INFIT'AH — ٨ – الإِنْفِتَاحُ

Kilugha ni kuwa mbali mbali, katika Qur'ani ni kuacha ulimi kutokana na sehemu ya juu ya kinywa inapotoka herufi ya munfatih na herufi zake ni zile zisizokuwa za Al – Ittbaq.

9. AL – IDH'LAAQ — ٩ – الإِذْلاَقُ

Kilugha ni Fasaha na wepesi wa kuitamka herufi kwenye ulimi, katika Qur'ani, ni utegemevu wa herufi unapoitamka kwenye ncha ya ulimi na mdomo na herufi zenyewe: ف – ر – م – ن – ل – ب Zimekusanywa na kusemwa (فِرَّ مِنْ لَبْ).

10. Al- ISSMA'T — ١٠ – الإِصْمَات

Kilugha maana yake 'kuzuia', katika Qur'ani ni uzito wa kutamka herufi; na herufi zake ni zile zisizokuwemo katika Al – Idh'laq.

## TUJIKUMBUSHE

الصِّفَاتُ المتضادَّة

SIFA ZENYE KINYUME CHAKE

Nazo ni kumi (10):

| | | |
|---|---|---|
| AL HAMS | DHIDI YAKE | AL JAHR |
| ASH-SHIDDAH | DHIDI YAKE | ARRAKHAWAH |
| ATTAWASSUT | | |
| AL ISTIILAA | DHIDI YAKE | AL ISTIFA'L |
| AL ITTBA'Q | DHIDI YAKE | AL INFITAH |
| AL IDH'LAAQ | DHIDI YAKE | AL ISMA'T |

| HERUFI ZAKE: 1. AL HAMS | DHIDI YAKE | 2. AL JAHR |
|---|---|---|
| الهَمْسُ<br>HERUFIZAKE<br>(فحثَّه شخصٌ سَكَت)<br>YAANI:<br>ف – ح – ث – هـــ – ش<br>-خ – ص – س – ك – ت | | الجَهْرُ<br>HERUFIZAKE<br>Zote zile zisizokuwa za AL HAMS. Nazo ni<br>أ – ب – ج – د – ذ – ر – ز<br>– ض – ط – ظ – ع – غ –<br>ق – ل – م – ن – و – ي |
| 3. AS-SHIDDAH | DHIDI YAKE | 4. ARRAKHAWAH |
| الشِّدَّة<br>HERUFI ZAKE<br>(أَجِدْ قطٍ بَكَتْ)<br>YAANI<br>أ – ج – د – ق – ط<br>ب – ك – ت<br>NA: ATTAWASSUT<br>التوسُّطُ<br>HERUFI ZAKE<br>(لِن عُمَر)<br>YAANI<br>ل – ن – ع – م – ر | | الرَّخاوة<br>HERUFI ZAKE ZISIZO-KUWA ZA AS-SHIDDAH NA ATTAWASUTU<br>NAZO NI<br>ث – ح – خ – ذ – ر – ز –<br>س – ش – ص – ض – ظ –<br>ع – غ – ف – هـــ – و – ي |

| 5. AL- ISTIILAA | DHIDI YAKE | 6. AL- ISTIFA'L |
|---|---|---|
| الاستعلاءُ<br>HERUFI ZAKE<br>(خُصَّ ضَغْطٍ قِظْ)<br>YAANI<br>خ– ص – ض – غ–<br>ط– ق – ظ | | الاستفالُ<br>HERUFI ZAKE ZISIZO-KUWA ZA ISTIILAA:<br>ا– ب – ت – ث – ج – ح – خ – د<br>ذ – ر – ز – س – ش – ع – ف<br>ك – ل – م – ن – هـ – و – ي |
| 7. AL- ITTBA'Q | DHIDI YAKE | 8. AL INFITA'H |
| الإطباقُ<br>HERUFI ZAKE<br>(ص – ض – ط – ظ) | | الإنْفِتَاحُ<br>HERUFI ZAKE ZISIZO-KUWA ZA AL- ITTBA'Q:<br>أ– ب – ت – ث – ج – ح–خ– د<br>ذ – س – ش – ع – غ– ف – ق<br>ك – ل – م – ن – هـ – و – ي |
| 9. AL- IDH'LAAQ | DHIDI YAKE | 10. AL- ISSMA'T |
| الإذِلاقُ<br>HERUFI ZAKE<br>(فِرَّ مِنْ لَبْ)<br>YAANI<br>ف – ر – م – ن–<br>ل– ب | | الإصماتُ<br>HERUFI ZAKE ZISIZOKU-WA ZA AL- IDH'LAAQ:<br>أ– ت – ث – ج – ح – خ – د – ذ<br>ز – س – ش – ص – ض – ط – ظ<br>ع – غ – ق – ك – هـ – و – ي |

DARSA YA KUMI NA NNE

## صفات الحروف (٣)

**قال تعالى**

لِإِيلَٰفِ قُرَيۡشٍ ﴿١﴾ إِۦلَٰفِهِمۡ رِحۡلَةَ ٱلشِّتَآءِ وَٱلصَّيۡفِ ﴿٢﴾
فَلۡيَعۡبُدُواْ رَبَّ هَٰذَا ٱلۡبَيۡتِ ﴿٣﴾ ٱلَّذِيٓ أَطۡعَمَهُم مِّن جُوعٖ
وَءَامَنَهُم مِّنۡ خَوۡفِۭ ﴿٤﴾

## SIFA ZA HERUFI (2)

Sifa ambazo hazina kinyume chake na ambazo zinaitwa kwa Kiarabu Assifaat gheiril Mutadhadah

**الصِّفَاتُ غَيْرِ المُتَضَادَّة**

Nazo ni Sifa saba (7):

1. ASSAFEER — ١– الصَّفِيْرُ

Kilugha sauti ya kifirimbi ambayo hulia baadhi ya ndege kama kifirimbi. Katika Qur'ani ni sauti zaidi inayotoka kwenye midomo miwili unapozitamka herufi zake, nazo ni

**ص– س– ز (الصاد والسين والزاي)**

2. AL- QALQALA — ٢– القلقلة

Kilugha: Mtikisiko au kutaharaki, katika Qur'ani ni sauti zaidi inayotoka kwenye Makh'raj baada ya kuitoa herufi kwa nguvu na imeitwa hivyo kwa sababu ulimi unatikisika (kutokana mahala pake) unapozitamka herufi zake nazo ni herufi tano:

**ق– ط– ب– ج– د.**

Wataalamu wameziweka pamoja hivi: **(قُطْبِ جَدْ)**

Kuna ayna mbili za Qalqala nazo ni:

<u>Qalqala Ndogo</u> — **أ– قلقلة صغرى**

Herufi zake zinapokuwa katikati ya neno zinakuwa na sukun k.m. (يَبْدَأُ – يَقْتُلُونَ) - Ba (ب) na Qaf (ق) zina sukun katikati ya maneno.

Qalqala Kubwa ب– قَلقَلَة كُبْرَى

Zinapotiwa herufi za Qalqala sukun mwisho wa neno kama: (عَذَابْ – عَلَقْ)

**3.** ALLIN ٣– اللِّيْن

Maana yake kilugha ulaini (dhidi yake ugumu), na kwa elimu ya Qur'ani ni WAW au YA zilizotiwa sukun; na herufi zilizo kabla yao zina fat'ha na husimama baada yake (hizo herufi: و– ي) kwa sukun. Na zimeitwa hivyo kwa kutoka kwake kwa wepesi, bila ya taklifu ulimini. Kwa mfano: (Khawf – bayt) خَوْف - بَيْت

4. AL- INHIRAAF ٤– الإِنْحِرَافُ

Maana yake kilugha kilichokaa upande au kujipinda, kupotoka kwa Kiarabu huitwa 'Mayl' – (المَيلُ) Amma kwa elimu ya Qur'ani: Kwendea herufi baada ya kutoka kwake kwenye ncha ya ulimi mpaka Makh'raj nyengine. Herufi zenyewe ni (اللام والراءُ) Lam na Ra. Zimeitwa hivyo kwa sababu zinapotamkwa hutoka kwenye Makh'raj yao na kwenda kwenye ncha ya ulimi. (Kwa Kiarabu huitwa zimepotoka) kwa kuacha Makh'raj yao na kwenda Makh'raj ya herufi nyengine.

5. ATTAKREER ٥– التكرير

Maana yake kwa lugha ya kiarabu kukariri, yaani kurejea mara moja au zaidi na kwa elimu ya Tajwid-el Qur'an ni kukariri ulimi unapotamka herufi, nayo ni herufi moja; nayo ni Ra الراءُ

Na haijuzu kutoa zaidi ya Ra moja. Na namna ya kuitamka kwa uangalifu ni kuambatisha mgongo wa ulimi na sehemu ya juu ya kinywa (kaa, kakaa, la kinywa) muambatanisho thabiti, na tamko lake liwe mara moja.

6. ATTAF'SHY ٦– التفشي

Maana yake kwa lugha ni kuenea. Na kwa elimu ya Tajweed ni kuenea kwa hewa ndani ya kinywa unapoitamka herufi yake nayo ni 'Shin' (الشين) Na imeitwa hivyo kwa kuenea kwake katika kinywa.

## 7. AL- ISTITTALA                                        ٧- الاستطالة

Kilugha maana yake kunyooka (kwa urefu) Ama kwa elimu ya Tajweed ni kuivuta sauti kutoka mwanzo wa ulimi mpaka mwisho wake na herufi yake ni 'Dhad' (الضاد)

Na baada ya kuelezea juu ya sifa zenye kinyume chake na zisizo kinyume chake imetudhihirikia kwamba kila herufi haina budi kusifika kwa uchache kwa sifa tano zenye kinyume chake tena huwenda zikasifika kwa sifa moja au mbili zisizo na kinyume chake au zisiwe na sifa yo yote katika hizo zisizo kinyume chake.
Tuangalie Jadweli ya Sifa zote za alphabeti za Kiarabu tokea Alifu mpaka Ya:

JADWELI YA SIFA ZA HERUFI ZOTE ZA KIARABU

جَدولَ صفَاتُ الحُروفُ الهجَائيَةَ

| | | SIFA ZISIZO NA KINYUME الصفات غير المتضادة | | | | | | | SIFA ZENYE KINYUME CHAKE الصفات المتضادة | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| JUMLA YA SIFA مجموع الصفات (KWA KILA HERUFI) | | 7 الاستطالة | 6 التفشي | 5 التكرير | 4 الانحراف | 3 اللين | 2 القلقلة | 1 الصفير | 10 الإصمات | 9 الإذلاق | 8 الانفتاح | 7 الإطباق | 6 الاستفال | 5 الاستعلاء | 4 التوسط والرخاوة | 3 الشدة | 2 الجهر | 1 الهمس | HERUFI الحروف |
| 5 | ٥ | | | | | | | | * | | * | | * | | | * | * | | أ |
| 6 | ٦ | | | | | | * | | | * | * | | * | | | * | * | | ب |
| 5 | ٥ | | | | | | | | * | | * | | * | | | * | | * | ت |
| 5 | ٥ | | | | | | | | * | | * | | * | | * | | | * | ث |
| 6 | ٦ | | | | | | * | | * | | * | | * | | | * | * | | ج |
| 5 | ٥ | | | | | | | | * | | * | | * | | * | | | * | ح |
| 5 | ٥ | | | | | | | | * | | * | | | * | * | | | * | خ |
| 6 | ٦ | | | | | | * | | * | | * | | * | | | * | * | | د |
| 5 | ٥ | | | | | | | | * | | * | | * | | * | | * | | ذ |
| 7 | ٧ | | | * | * | | | | | * | * | | * | | * | | * | | ر |

| | | SIFA ZISIZO NA KINYUME الصفات غير المتضادة | | | | | | | SIFA ZENYE KINYUME CHAKE الصفات المتضادة | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| JUMLA YA SIFA مجموع الصفات (KWA KILA HERUFI) | | 7 | 6 | 5 | 4 | 3 | 2 | 1 | 10 | 9 | 8 | 7 | 6 | 5 | 4 | 3 | 2 | 1 | HERUF I الحروف |
| | | الاستطالة | التفشي | التكرير | الانحراف | اللين | القلقلة | الصفير | الإصمات | الإذلاق | الانفتاح | الإطباق | الاستفال | الاستعلاء | التوسط والرخاوة | الشدة | الجهر | الهمس | |
| 6 | ٦ | | | | | | | * | * | | * | | * | | * | | * | | ز |
| 6 | ٦ | | | | | | | * | * | | * | | * | | * | | | * | س |
| 6 | ٦ | | * | | | | | | * | | * | | * | | * | | | * | ش |
| 6 | ٦ | | | | | | | * | * | | | * | | * | * | | | * | ص |
| 6 | ٦ | * | | | | | | | * | | | * | | * | * | | * | | ض |
| 6 | ٦ | | | | | | * | | * | | | * | | * | | * | * | | ط |
| 5 | ٥ | | | | | | | | * | | | * | | * | * | | * | | ظ |
| 5 | ٥ | | | | | | | | * | | * | | * | | * | | * | | ع |
| 5 | ٥ | | | | | | | | * | | * | | | * | * | | * | | غ |
| 5 | ٥ | | | | | | | | | * | * | | * | | * | | | * | ف |
| 6 | ٦ | | | | | | * | | * | | * | | | * | | * | * | | ق |
| 5 | ٥ | | | | | | | | * | | * | | * | | | * | | * | ك |
| 6 | ٦ | | | | * | | | | | * | * | | * | | * | | * | | ل |
| 5 | ٥ | | | | | | | | | * | * | | * | | * | | * | | م |
| 5 | ٥ | | | | | | | | | * | * | | * | | * | | * | | ن |
| 5 | ٥ | | | | | | | | * | | * | | * | | * | | | * | هـ |
| 6 | ٦ | | | | | * | | | * | | * | | * | | * | | * | | و |
| 6 | ٦ | | | | | * | | | * | | * | | * | | * | | * | | ي |

MFANO:

(1)(أ) yaani Alif ina sifa 5 zenye kinyume chake. Lakini haina sifa zisizo na kinyume chake. Sifa hizo 5 ni: AL- JAHR – ASH-SHIDDAH – AL- ISTIFAAL – AL- INFIT'AH – AL- ISSM'AT.

(2) (Ra) الراء ina sifa 5 zenye kinyume chake. Nazo ni: AL- JAHR – ATTAWASSUT – AL- ISTIFA'L – AL- INFIT'AH – AL- ADH'LAAQ. Na sifa 2 zisizo kinyume chake nazo: AL- INHIRAAF – ATTAKREER. Kwa hivyo Ra ina jumla ya sifa 7.

الهمس
الجهر
الشدة
الاستعلاء
الاستفال
الإطباق
الانفتاح
الأذلاق
القلقلة
اللين
التكرير

الإصمات
التوسط والرخاوة
الصفير
الانحراف
الاستطالة

DARSA YA KUMI NA TANO

# إدغام المتماثلين والمتجانسين والمتقاربين

**قال الله تعالى**

١– أَيْنَمَا تَكُونُوا يُدْرِككُّمُ الْمَوْتُ وَلَوْ كُنتُمْ فِي بُرُوجٍ مُّشَيَّدَةٍ
(النساء – ٧٨)

٢– يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُونُوا أَنصَارَ اللَّهِ كَمَا قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ
لِلْحَوَارِيِّينَ مَنْ أَنصَارِي إِلَى اللَّهِ قَالَ الْحَوَارِيُّونَ نَحْنُ أَنصَارُ اللَّهِ
فَآمَنَت طَّائِفَةٌ مِّن بَنِي إِسْرَائِيلَ وَكَفَرَت طَّائِفَةٌ فَأَيَّدْنَا الَّذِينَ
آمَنُوا عَلَى عَدُوِّهِمْ فَأَصْبَحُوا ظَاهِرِينَ ﴿١٤﴾ (الصف – ١٤)

٣– وَقُل رَّبِّ زِدْنِي عِلْمًا ﴿١١٤﴾ (طه – ١١٤)

Tukisoma jina la darsa yetu hii tutaona namna tatu za Id'gham:

1. Kwanza Id'gham al Mutamathilayn yaani Id'gham zenye kufanana (nazo ni namna mbili).
2. Id'gham al Mutajaanisayn yaani Id'gham zenye kufanywa ziwe namna moja.
3. Id'gham al Mutaqaribayn yaani zenye kukaribiana ( yaani zinakaribiana kuwa namna moja). Nazo ni mbili.

Tukianzia Aya ya kwanza katika neno hili (يُدْرِككُّمُ) Utaona Kaf ya kwanza ina sukun na imeingizwa katika Kaf ya pili na kuwa herufi moja tu Kaf iliyokazwa au iliyotiwa shadda na kutamkwa Yudrikkumu – يُدْرِكُّمُ.

Katika Misahafu utaona herufi zenye kuingizwa na herufi nyengine hazitiwi sukun huachwa tupu kukufahamisha herufi hizi hazitamkwi katika Id'gham na Ikhfaa. Hutiwa sukun katika Idh'haar tu.

Id'gham hii inaitwa Id'gham Mutamathilayn إدغام متماثلين kwa sababu herufi mbili ni za namna moja Kaf na Kaf zote zinatoka kwenye Makh'raj moja na sifa zao namna moja.

Mifano mengine yenye kufanana ni hii:

(اذهب بِّكتابي – في قلوبهم مَّرض – قل لَّهم)

Lam + Lam    Mim + Mim    Ba + Ba

Katika Aya ya pili tunaona katika neno (فَـــئـامَنَتْ) Ta yenye sukun imeingizwa katika ' ط' yenye haraka, nayo ina fat'ha na kutamkwa herufi hizo (ط + ت) kuwa herufi moja yenye shadda au mkazo katika herufi ya neno la pili na hutamkwa (Fa'amanattaifatun). Muingizo huo wa herufi mbili kuwa moja huitwa إِدْغَامُ مُتَجَانِسَيْنِ kwa sababu zimekuwa jinsi moja kwa kuungana kwao na zinatoka kwenye Makh'raj moja lakini zinakhitalifiana kwa sifa. Id'gham ya namna hii inakhusika na Makhaarij tatu:

1. AL HUROOFU ANNATT'IYA    ١– الحروف النَّطعيَّة (ت– د– ط)

Herufi hizo juu tatu zinatoka kwenye Makh'raj ya sehemu ya juu ya kinywa ambayo huitwa Kaakaa au kaa la kinywa na inapasa Id'gham iwe mahali panne:

(a) Kuunganika    أ– إِدغَام الدَّالِ في التَّاءِ مثلُ: (قَد تَّبَيَّنَ–عَبَّد تّ)

Dal (د) katika Ta (ت) na kutamkwa herufi moja ya (Ta) yenye shadda. Tunasema kwenye mifano ya juu "Qa'ttabayyana" "Abba'tta" (tumeonyesha (tt) kuonyesha kukaza kwa (shadda)

(b)Kuingia Ta (ت) katika Dal (د)    ب– إِدغامُ التاءِ في الدّالُ

mfano:    مثلُ: (أَجِيبَت دَّعوا)

(c)Kuingia (Ta - ت) katika (Tta – ط)    ج– إِدغامُ التاءِ في الطاءِ مثلُ:

Mifano: Hamattaifatan - Kafarattaifatan.    (هَمَّت طَّائِفَةً – كفرت طَّائِفَةً)

(d)Kuingia (ط) katika (ت) lakini    د– إدغامُ الطاءِ في التاءِ مثلُ:

Id'gham yake imepungua kwa sababu inabakia athari ya (ط)

Mifano: Farattu – Basatta    (فَرَطــتُّ – بَسَطــتَّ)

2. AL- HURUFUL LITHAWIYYAH (ث– ذ– ظ): الحروف اللثوية –٢

Nazo ni herufi zinazotoka baina ya ncha ya ulimi na ncha za meno mawili ya mbele ya juu. Na inapasa Id'gham Dhali (ذ) katika (ظ) kwa mfano: (إِذ ظَّلَمْتُمْ).

Na vile vile Id'gham (ث) katika (ذ) kwa mfano: (يَلْهَـث ذَّلِـك) na mfano ni huu tu katika Qur'ani.

3. AL- HURUFU ASHAFAWIYAH (ب– م) الحروف الشفوية –٣

Herufi zinazotoka baina ya midomo miwili Ba na Mim. Inatakikana iwe Id'gham katika maudhuu moja, nayo ni kuingiza (ب) katika (م) katika pahala pamoja katika Qur'an, nako ni –

(يَابُنَيَّ إِرْكَب مَّعَنَا)

Ama katika Aya ya tatu imeingizwa (Id'gham) Lamu yenye sukun katika neno (وقل) katika Ra (ر) yenye haraka nayo ni fat'ha katika neno (رَّبِّ) na zikatamkwa kwa Ra yenye shadda (رَّ) na huitwa ID'GHAM MUTAQARIBAYN إِدْغَم مُتَقَارِبَيْن Kwa sababu herufi mbili zinakaribiana katika Makh'raj na zinakhitilafiana katika sifa. Nazo ni namna mbili.

(a) Id'gham (ل) katika (ر) mfano: أ– إِدْغَمُ اللاَّم في الراءِ: مثال

(بَل رَّفَعَهُ)

(b)Id'gham (ق) katika (ك) mfano: ب– إِدْغَمُ القافِ في الكافِ: مثال

(أَلَمْ نَّخْلُقـكُّم)

Namna hii ya Id'gham inajuzu kuwa kamili kwa kutamka (ك) tupu yenye shadda na inakuwa pia Id'gham iliyopungua kwa kubakia athari ya (ق) huwa tafkhim (inajaa kinywa). (Tutajifunza zaidi juu ya mkazo huo katika darsa zijazo.

## TUJIKUMBUSHE

1. ID'GHAM AL MUTAMATHILAYN ni kuunganika herufi mbili zenye Makh'raj moja na sifa moja.
2. ID'GHAM AL MUTAJANISAYN ni kuwafikiana herufi mbili katika Makh'raj moja na kukhitalifiana katika sifa.
3. ID'GHAM AL MUTAQARIBAYN ni zinakaribiana herufi mbili Makhaarij zao lakini zinakhitalifiana sifa.

DARSA YA KUMI NA SITA

# الحروف النورانية

**قال الله تعالى:**

كٓهيعٓصٓ ﴿١﴾ ذِكْرُ رَحْمَتِ رَبِّكَ عَبْدَهُۥ زَكَرِيَّآ ﴿٢﴾ (مريم ١-٢)

طه ﴿١﴾ مَآ أَنزَلْنَا عَلَيْكَ ٱلْقُرْءَانَ لِتَشْقَىٰٓ ﴿٢﴾ (طه ١-٢)

## AL- HURUFU ANNURANIYAH

Katika mianzo ya baadhi ya Sura za Qur'an zipo baadhi ya herufi. Zipo kauli mbali mbali katika kufasiri maana yake au makusudio yake. Kuna wenye kusema kuwa ni majina ya Sura au ni katika Majina ya Mwenyezi-Mungu "Asmau Allahi Al Husna" na kuna wenye kusema kuwa Mwenyezi-Mungu Alishindana na watu katika kila zama na mahali walete Aya au Sura mfano wa hii Qur'ani iliyotungwa kwa mfano wa herufi hizi. Kiumbe hata akiwa mjuzi namna gani katika utungaji, itakuwa lengo lake ni kutunga hadithi au kasida au musiki. Ama Mola wa viumbe vyote Amefanya kutokana na herufi hizi Uongofu, Rehema na Uadilifu kwa wanadamu na Hukumu na Sharia na Aqida (Itikadi ya dini) na Ibada na Amefanya uhai kwa kila kilichomo katika maneno haya kina maana.

Ama idadi ya herufi hizi (za Nuraniyah) katika Mianzo ya Sura baada ya kuachwa zile zenye kukariri ni herufi kumi na nne (14) zimeekwa pamoja katika maneno. Nazo zinagawika katika sehemu tatu (3):

1. Sehemu ambayo haina Madda ndani yake nayo ni Alif.
2. Sehemu iliyofanywa kwa herufi mbili (2) Ya pili katika hizo ni Alif. Hii inavutwa haraka mbili na inaitwa **مدًّا طبيعياً حرفياً** ya Madda ya maumbile na ya herufi. Nayo ni yenye herufi tano:-

   **(حي طهر) (ر- هــ- ط- ي- ح)**

   na husomwa hivi **(حا- يا- طا- ها- را)**
3. Sehemu iliyofanywa kwa herufi tatu, kati yao herufi yenye Madda na hii inavutwa haraka sita bila ya kuzidisha au kupunguza. Kwa sababu hiyo ni Madda ya Lazima harfiyyi (ya herufi) kama tulivyokwisha kujifunza katika darsa za Madda au Mudood. Na herufi zake nane

   **(نقص عسلكم) – (ن- ق- ص- ع- س- ل- ك- م)**

Sehemu hii imegawika sehemu tatu au aina tatu:

A- LAZIM MUTHAQQAL HARFY أ- لاَزِمْ مُثَقَّل حَرْفِي

Inakuwa herufi ya tatu imeingizwa katika herufi inayoifuata mfano لاَم مِّيم katika (أَلٓمٓ) kwa sababu mwisho wa LAM ni Mim imeingizwa katika mim ya mwanzo kutokana na MIM (ميم).

B- LAZIM MUKHAFAF HARFY ب- لازم مخفف حرفي

Inakuwa herufi ya tatu ina sukun wala haingizwi pamoja na herufi ifuatayo kama Madda katika (قٓ –نٓ)

C- MAD LYN HARFY ج- مد لين حرفي

Herufi yake ni moja nayo ni (ع) Inavutwa kama Madda ya LYN kiasi cha haraka mbili au nne au sita.

## TUJIKUMBUSHE

HERUFI KATIKA Mianzo ya Sura ni kumi na nne (14) zilizowekwa pamoja katika (طَرَقَ سمعَك النَصيحة).

Sehemu kati yake haivutwi nayo ni Alif (الالف) na sehemu inavutwa haraka mbili herufi zake ni (حي طهر)
na sehemu inavutwa haraka sita inayoitwa Maddan Laziman Harfiyan (ya herufi) (مدّ الازما حرفيّاً)

Na herufi zake (نقص عسلكم)

isipokuwa herufi ya Ayn (ع) katika Sura ya Maryam na Ash'shura سورة مريم و الشورى
huvutwa haraka mbili au nne au sita kama Madda ya Allyn (مد اللين)

DARSA YA KUMI NA SABA

# التفخيم والترقيق

**قال الله تعلى:**

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ قُوٓا۟ أَنفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا وَقُودُهَا ٱلنَّاسُ وَٱلْحِجَارَةُ عَلَيْهَا مَلَـٰٓئِكَةٌ غِلَاظٌ شِدَادٌ لَّا يَعْصُونَ ٱللَّهَ مَآ أَمَرَهُمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ ٦ (التحريم)

## ATTAFKHEEM WA ATTARQEEQ

(a)Attafkheem: Kujaa kinywani yaani kuna baadhi ya herufi tukizitamka zinajaa kinywani, kwa mfano wa herufi ya (ق) Tukiangalia Aya ya Qur'ani juu tunaona neno ( قُوٓا۟) tukilitamka tunaona linajaa kinywa.

(b)Ama Attarqeeq ni kinyume cha herufi tulizozitaja juu nazo nyepesi kutamka wala hazijai kinywani, kwa mfano herufi hizi ziliomo katika neno (أَنفُسَكُمْ)

Kwa hivyo herufi za namna hizo zinagawika sehemu mbili. Herufi zinazojaa kinywani zinaitwa herufi MUFAKHAMAH مفخَّمة na zile zisizojaa kinywa zinaitwa herufi MURAQAQAH مرقَّقةٌ.

Attafkheem kwa lugha maana yake kuadhimisha lakini kwa elimu ya Tajweed ni uzito unaoingia herufi yaani sauti yake inapojaa kinywani

Attrqeeq: kilugha ni kinyume cha Attafkheem na kwa elimu ya Tajweed ni wepesi unaoingia herufi wala haijai kinywa.

Tafkheem inahusu herufi za Al- Istiilaa kama tulivyokwisha kujifunza katika darsa ya Sifa za Herufi nazo ukizitamka unanyanyuka ulimi na kufika kwenye sehemu ya juu ya kinywa, pamoja na herufi ya Ra (ر) katika baadhi ya hali zake na (ل) katika tamko la 'Allah' ikitanguliwa na dhamma au fat'ha. Ama herufi zilizobakia ni muraqaqa; nyepesi katika kinywa.

1. HERUFI ZA ISTIILAA حُرُوفِ إِسْتِعْلاَءِ

Nazo ni herufi hizi katika tamko la (خُصَّ ضَغْطٍ قِظْ) zote ni mufakhama مُفَخَّمَةٌ katika hali zake zote ila zinapokuwa zina kasra au sukun; baada ya kasra zinapungua uzito wake. Kwa mfano غِلاَظٌ (غِ) ni herufi ya Istiilaa na ina kasra kwa hivyo unapungua uzito wake kinywani.

2. HERUFI YA RA (ر) حَرْفُ الرَّاءِ

I Inakuwa (ر) yenye kujaa kinywa yaani mufakhama katika hali zifuatazo:

(a)Ikiwa (رُ) ina dhamma k.m. (يؤمِرُونَ – يبشِرُهم – رُزِقنا)

(b)Ikiwa (رَ) ina fat'ha k.m. (ورَبك – شرَاب – ناراً)

(c)Ikiwa (رْ) ina sukun na herufi iliyo kabla yake ina dhamma:

(قُرْآن – بِقُرْبَان – كالعُرْجون)

(d)Ikiwa (رْ) ina sukun na herufi iliyo kabla yake ina fat'ha:

(خَرْدل – قَرْيَة)

(e)Ikiwa (رْ) ina sukun na herufi iliyo kabla yake ina kasra Aridh. (yaani kasra isiyokuwa ya asili) (اِرْجعي – أَمِ ٱرْتابوا)

(f)Ikiwa ina sukun na herufi kabla yake ina kasra ya asili na baada ya herufi ya Istiilaa katika neno moja:

(قِرْطَاس – لَبِالْمِرْصَاد)

(g)Ikiwa (رْ) na herufi iliyo kabla yake ina sukun na kabla ya hiyo herufi yenye sukun, herufi ina fat'ha au dhamma:

(رْ) Ra ina sukun — Ra yenye sukun (رْ)

( القَدْرْ – الأُمُوْرْ )

Herufi ya kabla yake ina sukun nayo ni (وْ)

(مُ) Mim ina dhamma

Herufi kabla ya (دْ) ina fat'ha (قَ)

Herufi ya kabla yake (دْ)

**II** (Ra) inakuwa haijai kinywa, yaani Muraqaqa - **مُرَقَّقة**
katika hali zifuatazo:

(a)Ikiwa 'Ra' ina kasra (رِ) kwa mfano:(**رِجَالُ – مَرِيْج – فَضُرِب**)

(b)Ikiwa 'Ra' ina sukun (رْ) na herufi iliyo kabla yake ina kasra na ikiwa herufi iliyo baada yake si moja ya herufi ya Al Istiilaa (**خُصّ ضغطٍ قظْ**) k.m. (**فِرْعَوْن – وَاصْبِرْ**)

(c)Ikiwa 'Ra' ina sukun na herufi iliyo kabla yake ni 'Ya' yenye sukun k.m. (**خَبِيْرْ – خَيْرْ**)

(d)Ikiwa 'Ra' ina sukun imekuja baada ya herufi yenye sukun na kabla ya herufi yenye sukun; herufi ina kasra k.m.

(**حِجْرْ – السِّحْرْ**)

(e)Ikiwa herufi ya 'Ra' ina sukun na herufi iliyokuja kabla yake ina kasra ya asili na baada yake herufi ya Istiilaa katika neno la pili k.m. (**وأَنـــذِرْ قَوْمَكَ**)

Herufi ya Istiilaa (ق) katika neno la pili

(ذِ)ina kasra kabla ya Ra

(رْ) yenye sukun

3.( i )Inajuzu kutamka 'Ra' katika hali zote mbili zikiwa Mufakham au Muraqaqa katika:

(a)Ikiwa 'Ra' ina sukun (رْ) na herufi iliyo kabla yake ina kasra ya asili na herufi iliyo baada yake ni herufi ya Istiilaa yenye kasra k.m.

(**كل فِـــرْ قٍ**)

Herufi ya Istiilaa ina kasra

Herufi ya kabla ya 'Ra' ina kasra ya asili

'Ra' yenye sukun

(b)Ikiwa ‘Ra’ ina sukun (رْ) na kabla yake ipo herufi ya Istiilaa yenye sukun na kabla ya hiyo herufi ya Istiilaa, herufi ina kasra k.m.

‘Ra’ zenye sukun

Herufi ya kabla ya herufi ya Istiilaa yenye kasra (م)

(مِصْــرْ – القِــطْــرْ)

Herufi ya Istiilaa yenye sukun (طْ)

Herufi ya Istiilaa yenye sukun (صْ)

Herufi yenye kasra kabla ya herufi ya Istiilaa (ق)

3. ii –Lam katika tamko la jina la Mwenyezi-Mungu Mtukufu ‘ALLAH’ ٣– ii –لام لفظ الجلالة (الله)

‘Lam’ inakuwa mufakhama (yaani imejaa kinywani) ikitanguliwa na herufi yenye fat’ha au dhamma k.m.

(لا يعصونَ الله) – (ثُمَّ يُحْكِمُ اللهُ آيَاتِهِ)

Na huwa Muraqaqa yaani haijai kinywa na nyepesi kutamka ikitanguliwa na herufi yenye kasra k.m. (بِسْمِ اللهِ – اَلْحَمْدُ لِلَّهِ).

## TUJIKUMBUSHE

1. Hujaa kinywa (مفخمة) herufi za Istiilaa (خص ضغط قــظ) na 'Ra' katika baadhi ya hali zake na Lamu katika Tamko la Mwenyezi-Mungu ikitanguliwa na herufi yenye Fat'ha au Dhamma.
2. Huwa nyepesi kutamka (مرققــة) herufi za ISTIFAL na 'Ra' katika baadhi ya hali zake na Lamu katika Tamko la 'Allah' ikiwa imetanguliwa na herufi yenye kasra.

DARSA YA KUMI NA NANE

# التقاء ساكنين

**قال الله تعالى:**

إِذَا ٱلسَّمَآءُ ٱنشَقَّتْ ﴿١﴾
(الإنشقاق)

ٱللَّهِ ٱلَّذِى لَهُۥ مَا فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِى ٱلْأَرْضِ
(ابراهيم ٢)

وَأَقِيمُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ
( البقرة ٤٣)

يُسَبِّحُ لِلَّهِ مَا فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِى ٱلْأَرْضِ
(ابراهيم ١)

وَإِذْ قَالَ إِبْرَٰهِۦمُ رَبِّ أَرِنِى كَيْفَ تُحْىِ ٱلْمَوْتَىٰ
(البقرة ٢٦٠)

إِن تَرَكَ خَيْرًا ٱلْوَصِيَّةُ
(البقرة ١٨٠)

وَلَوْ أَنَّا كَتَبْنَا عَلَيْهِمْ أَنِ ٱقْتُلُوٓا۟ أَنفُسَكُمْ
(النساء ٦٦)

وَأَنَا۠ مَعَكُم مِّنَ ٱلشَّٰهِدِينَ ﴿٨١﴾
(ال عمران ٨١)

يَٰبَنِىٓ إِسْرَٰٓءِيلَ ٱذْكُرُوا۟ نِعْمَتِىَ ٱلَّتِىٓ أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ
(البقرة ٤٠)

فَتَمَنَّوُا۟ ٱلْمَوْتَ
(الجمعة ٦)

وَإِذْ فَرَقْنَا بِكُمُ ٱلْبَحْرَ
(البقرة ٥٠)

Tukiangalia Aya Tukufu za juu, tutaona kwamba zikikutanika herufi mbili zenye sukun, hapana budi na kuiondosha mojawapo katika hizo, kama ilivyoqaririwa katika Qawaid za lugha ya Kiarabu na kwa hivyo; ama iondoshwe herufi moja yenye sukun ya kwanza, au kuitia haraka (ama fat'ha, dhamma au kasra).

1. Kuondolewa herufi yenye sukun: ١– حذف الساكن

(a)Huondolewa herufi ya Madda Attabii (ا– و– ي) unapoendelea kusoma tu! Inapoangukia Hamzatel-Wasl baada ya herufi za Madda. Kuondoshwa huku ni kwa kuitamka tu, kwa sababu herufi iliyoondoshwa imethibitishwa katika Msahafu k.m. (angalia juu) " إِذَا ٱلسَّمَآءُ "

Idhaa – Alif imethibitishwa, lakini ukiitamka huivuti unaisoma Idha-ssamau.

Pia katika mfano wa pili (في) kuna ‘Ya’ mwisho huitamki ukaivuta Fii bali unasoma ‘Fi’; lakini imeandikwa, mfano: فِىٱلۡأَرۡضِ Pia katika ‘Wa aqimuu’ tunaisoma Wa aqimu-ssalata’ hatuivuti k.m. "وَأَقِيمُوا"

(b)Na pengine huweza kuondoshwa herufi yenye Madda ukiendelea kusoma au ukisimama kwa ajili kuondoshwa kwake kupo katika qiraa yetu hii "تُحْيِ ٱلْمَوْتَ" (ي) ya kuvutia tuhyii) imeondoshwa.

2. Kutia haraka herufi yenye sukun ٢– تحريك الساكن

(a)Hutiwa herufi yenye sukun ya kwanza kwa ‘KASRA’ ikiwa herufi yenye sukun ya kwanza mwisho wa neno la mwanzo ni mojapo ya herufi (لتنود) au tanween na herufi yenye sukun ya pili baada ya Hamzatel-Wasl k.m. " أَنِ ٱقۡتُلُوٓاْ " {Herufi ya kwanza yenye sukun ni nuni katika (أَنْ) imetiwa kasra (أَنِ) na herufi ya pili yenye sukun ni (قْ) ambayo baada ya Hamzatel-Wasl.}

Mfano mwengine " خَيۡرًا ٱلۡوَصِيَّةُ " Tunaposoma tunasema Khayranil-wassiyyatu "خَيْرَنِ ٱلْوَصِيَّةُ" nuni iliyoongezwa hapa badala ya tanween, ikiangukia baada ya tanween Hamzatel-Wasl; katika hali hii tunatia haraka hiyo nuni iliyoongezeka badala ya tanween kwa kasra; sharti iwe hiyo haraka katika hali ya kuendelea tu! Mfano mwengine "عَادًا ٱلأولى" tunasoma "عَادَنِ ٱلأولى"

(b)Hutiwa herufi yenye sukun ya kwanza kwa ‘FAT’HA’ ikiwa:

(i)Nuni katika (MIN – مِنْ) ikiangukia baada yake; Hamzatel-Wasl, k.m. "مِنَ ٱلشَّاهِدِيْنَ"

(ii)Ya ya mwenye kusema inayoitwa (يَاءُ المُتَكَلِّمُ) ikiangukia baada yake Hamzatel-Wasl k.m. نِعْمَتِيَ ٱلَّتِي

(c)Hutiwa herufi yenye sukun ya kwanza kwa ‘<u>DHAMMA</u>’ ikiwa:

(i)Waw - Allyn ikiangukia baada yake Hamzatel-Wasl. k.m.

" فَتَمَنَّوُا۟ ٱلْمَوْتَ "

(ii)<u>Mim</u> yenye kuonyesha <u>wingi</u> ambao huitwa (ميم الجمع)

ikiangukia baada yake Hamzatel-Wasl: بِكُمُ ٱلْبَحْرَ (Asili yake بكُمْ , ilivyokuwa imefuatiwa na Hamzatel-Wasl (ٱ) imetiwa dhamma badala ya sukun.

## DARSA YA KUMI NA TISA

## الوقف والابتداء

### KUSIMAMA NA KUANZA
### SEHEMU YA KWANZA

1. Katika Hadithi ya Ummu Salama (Mke wa Mtume S.A.W.) Radhi za Mwenyezi Mungu juu yake – kuwa Mtume S.A.W. Alipokuwa Akisoma Qur'ani Akikata kusoma kwaKe Aya Aya Akisoma hivi:

   Akisita بِسْمِ اللهِ الرَّحْمَـٰـنِ ٱلرَّحِيمْ Akisita ٱلْحَمْدُ للهِ رَبِّ ٱلْعَالَمِينْ

   Akisita الرَّحْمَـٰـنِ ٱلرَّحِيمْ Akisita مَـٰـالِكِ يَوْمِ ٱلدِّينْ

   na hivyo hivyo kila baada ya Aya.

   Ameisimulia Hadithi hiyo: رواه أبو داود والترمذي وأحمد وغيرهم

   Abu Daud na Attirmidhy na Ahmed na wengineo.

2. Ameulizwa Sayyidna Ali Bin Abi Talib Radhi za Mwenyezi-Mungu juu yake katika Qauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: (وَرَتِّلِ ٱلْقُرْآنَ تَرْتِيلاً)

   Akajibu (هو تجويدُ الحروفِ ومعرفةُ الوقوفِ) Yaani Kuzisoma vyema herufi na kujua pa kusimama.

   Kujua wapi pa kusimama, ndiyo ubingwa wa elimu ya Tajweed. Kusimama pahali pake kunasaidia kufahamu maana ya Aya. Ama kusimama pasipo mahali pake huwenda kukageuza maana ya Aya au kuutia kombo uzuri wa usomaji wa Qur'ani. Na ni jambo linalojulikana vyema katika kusimama ni kwa kutia sukun herufi ya mwisho.

   Kwa sababu ni kawaida ya Waarabu hawasimami kwenye herufi yenye haraka (fat'ha au dhamma au kasra). Tunaiita herufi mutaharik wala hawaanzi kwa herufi yenye sukun.

Ulamaa wa elimu ya Tajweed wameigawa sehemu kadha lakini zilizo muhimu ni hizi zifuatazo:

1. MSIMAMO ULIYOTIMIA (AL WAQF-ATTAM) ١ – الوَقْفُ التَّامَ

   Nao ni msimamo kwenye neno lisilo na uhusiano na neno lijalo baada yake wala lililo kabla yake si kwa tamko wala maana na zaidi huwa mwanzo wa Aya na kumalizika qisa. Kwa mfano:

   ( أُولَٰٓئِكَ عَلَىٰ هُدًى مِّن رَّبِّهِمْ ۖ وَأُولَٰٓئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ٥ –
   مَٰلِكِ يَوْمِ الدِّينِ - وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ )

Nayo huwa mwisho wa qisa au mwisho wa sura, au kusimama kabla ya <u>Ya</u> ya Kuita يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ Surat el-Hujuraat Aya (1).

Au kitendo cha kuamrisha ﴿ قل: ٱنتَظِرُوٓاْ إِنَّا مُنتَظِرُونَ ﴾ Suratel-Anaam Aya (258).

Na Lamu ya Kuapa لَآ أُقۡسِمُ بِيَوۡمِ ٱلۡقِيَٰمَةِ Suratel-Alqiyama Aya (1) au Lamu ya Sharti au kupambanua baina Aya ya Rehema na Aya ya Adhabu na kusimama kwenye makatazo au kumalizika maneno.

وَإِذۡ تَأَذَّنَ رَبُّكُمۡ لَئِن شَكَرۡتُمۡ لَأَزِيدَنَّكُمۡۖ وَلَئِن كَفَرۡتُمۡ إِنَّ عَذَابِي لَشَدِيدٞ ٧

Mfano wa Lamu ya Sharti "Lain'shakartum Laazidannakum" Yaani 'Nitakuzidishieni (Kheri) lakini Sharti Munishukuru'.

## 2. MSIMAMO WENYE KUTOSHELEZA ٢- الوقف الكافى

Nao ni msimamo kwenye neno lisilo na uhusiano na neno lililo baada yake wala la kabla yake kwa kutamka lakini lina uhusiano kwa maana, na msimamo huo zaidi katika mgawanyiko wa vifungu vya Qur'ani na kwengineko kama kusimama kwenye neno (لا يؤمنونَ) katika Qauli yaKe Mwenyezi-Mungu

Inapendeza kusimama hapa ( ءَأَنذَرۡتَهُمۡ أَمۡ لَمۡ تُنذِرۡهُمۡ لَا يُؤۡمِنُونَ )

na vile vile inapendeza kuanza na Aya inayokuja baada yake.

## 3. MSIMAMO MZURI ٣- الوقف الحسن

Nao ni msimamo kwenye neno lenye uhusiano na yaliyo baada yake au kabla yake katika matamshi na maana pia kama kusimama kwenye (بسم الله) na kwenye الحَمْدُ لِلَّه lakini kuanzia kwa yaliyo baada yake ambayo yanahusiana na mwanzo wake haipendezi ijapokuwa inajuzu kusimama lakini kuanza yaliyo baada yake haipendezi.

k.m. kusimama بسم الله lakini kuja kuanzia الرحمن الرحيم bila ya mwanzo wake haipendezi n.k.

## 4. MSIMAMO UNAOCHUKIZA ٤- الوقف القبيح

Nao ni kusimama kwenye maneno yasiyotimia maana yake au kukata kwenye sehemu ya mwanzo ya maneno pasina kueleza habari yake n.k. Kunachukiza zaidi kusimama kwenye sifa isiyolingana na udhati wa Mwenyezi-Mungu. Kama kwa mfano kusimama ( لَا يَسۡتَحۡيِۦٓ ) kwenye Qauli yaKe Taala. Haifai

kusimama ila kwa dharura kisha urejee kwenye neno ulilolisimamia ( لَا يَسْتَحْيِۦٓ أَن يَضْرِبَ مَثَلًا ) ili isibadilike maana, urejee inakopendeza kuanza.

## KUANZA الا بتداءُ

Ni juu ya msomaji Qur'ani, kama alivyosimama msimamo mzuri inapasa na kuanza kwake kuwe kuzuri.
Asianze ila kwa yanayoweka wazi maana. Kwa hivyo kama ilivyokuwa kuna msimamo mbaya vile vile kuna kuanza kubaya kama katika kusoma Aya hii:- ( وَقَالَتِ ٱلْيَهُودُ يَدُ ٱللَّهِ مَغْلُولَةٌ ) wewe ukienda kuanzia ( يَدُ ٱللَّهِ مَغْلُولَةٌ ) sivyo hivyo kabisa!

## TUJIKUMBUSHE

Kujua pa kusimama ni ubingwa wa elimu ya Tajweed. Katika sehemu zake zilizo muhimu kabisa ni:-
MSIMAMO ULIOTIMIA: Nao ni msimamo uliotimia maana yake wala hauna alaqa na maneno yaliyo baada yake la kwa matamshi wala maana.
MSIMAMO WENYE KUTOSHELEZA: Nako ni kusimama palipotimia maana yake na penye alaqa na yanayofuata kwa maana si matamshi.
MSIMAMO MZURI: Nako ni kusimama palipotimia maana yake na pana alaqa na yanayofuata kwa matamshi na maana.
MSIMAMO MBAYA: Nako ni kusimama pasipotimia maana yake na kuna alaqa na yafuatayo kwa matamshi na maana.
Mifano: ( لَا تَقْرَبُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَأَنتُمْ سُكَٰرَىٰ )
Kama katika Aya hii kusimama kwenye neno ( ٱلصَّلَوٰةَ ) ni vibaya kabisa kunaleta maana siyo (musikaribie Sala) vipi!? Inabidi uimalize ilete maana sahihi.
Mfano mwengine wa ( وَقَالَتِ ٱلنَّصَٰرَى ٱلْمَسِيحُ ٱبْنُ ٱللَّهِ )
Kuanzia mahala pabaya ukianzia kwenye neno ( ٱلْمَسِيحُ ) utakuwa umekufuru.
Basi lazima tutahadhari na tujue pa kuanzia na pa kusimamia barabara.

## DARSA YA ISHIRINI

# الوقف والابـتـداء (٣)

## KUSIMAMA NA KUANZA
## (SEHEMU YA 2)

Humtokelea msomaji; kwa ajili ya kikohozi au kumpaa pumzi kukamlazimikia kusimama (pasina kusudi) kwa hivyo inawezekana kusimama kwenye neno lolote lakini ni juu yake kurejea nyuma kidogo pale aliposimama kisha aendelee kusoma (ili isipotee maana ya Aya) na msimamo huu huitwa 'Msimamo usio na budi' الوقف الاضطراري

au hutumiwa kwa kumfanyia mwanafunzi mtihani kwa kujaribiwa na mwalimu wake, husimama kisha hurejea nyuma na kuunga na pale aliposimama ikiwa si mahali pa kusimama na huu huitwa Msimamo wa majaribio (au mtihani) الوقف الاختباري

Ni makosa kusimama katikati ya neno, ila mwisho wa neno; juu ya haya inapasa kuchunguza Maelezo ya Msahafu wa Othman uitwao رسمِ المصحفِ العثماني (ambao ndio unaotumika sasa) na itakuwa sawa pindi ukikubaliana na mpango unaojulikana (katika Msahafu huo) au ukikhalifu.

1. Ikiwa kuna vipande vya maneno katika maelezo ya Rasm tunasimama kwenye kipande cha mwisho (au maq'tooi ya mwisho) ikiwa hakuna budi au kwa ikhtibar (mtihani).

   Kwa mfano: (إِن مَّا). Imetajwa katika Qur'an Tukufu kipande katika mawdhuu moja nayo ni (وَإِن مَّا نُرِيَنَّكَ) inajuzu kusimama au kwenye (إِن) au kwenye (ما) msimamo usio na budi au msimamo wa majaribio na kwa mfano mwengine wa (عن ما) katika ((عَن مَّا نُهُوا عَنْهُ)) Sura Al Aaraaf Aya 166. Inajuzu kusimama kwenye (عن) au kwenye (ما) kama juu. Vile vile mifano mengine

(ومن ما): (( هَل لَّكُم مِّن مَّا مَلَكَتْ أَيْمَٰنُكُم مِّن شُرَكَآءَ )) سورة الروم الاية ٢٨

وفي (( فَمِن مَّا مَلَكَتْ أَيْمَٰنُكُم مِّن فَتَيَٰتِكُمُ ٱلْمُؤْمِنَٰتِ )) سورة النساء الآية٢٥

2. Ikiwa maneno yameungana kama neno moja katika maelezo (yaani ya rasm) tunasimama mwisho wa muungano (wa

maneno hayo), mfano:

Neno ‘Imma’ haijuzu kusimama **(إِما): نحو ﴿وَإِمَّا تَخَافَنَّ﴾**
baada ya neno hili, bali usimame mwisho wa maneno mawili ya juu. Na mfano wa ‘Amma’ kwenye neno ‘Amma yushrikun’ haijuzu kusimama kwenye ‘Amma’ **(عما) نحو ﴿عَمَّا يُشْرِكُونَ﴾**
Na mfano kwenye neno ‘Biisamaa’ haijuzu kusimama hapo bali uendelee mpaka mwisho wa maneno: k.m.

**(بئسما) نحو ﴿بئسما اشتَروا به أَنفسهم﴾**

3. Ikiwa herufi za Madda mwisho wa neno ni thabiti kwa hivyo ni juu yetu kuithibitisha pia. K.m. ( يَٰٓأَيُّهَا )
   Kwenye Aya hii ( يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَوۡفُواْ بِٱلۡعُقُودِۚ ).
   mfano mwengine **(وقالا)** kwenye ( وَقَالَا ٱلۡحَمۡدُ لِلَّهِ ) tunasimama kwenye Alif ya kuonyesha watu wawili inaitwa **أَلَفِ التَّثْنِيَةِ** lakini inakuwa haitamkwi tukiendelea kusoma “Waqalal Hamdulillahi”
   Mfano mwengine kama wa juu: **(ذَاقَا)** tunaivuta ‘Dhaqaa’ (haraka 2) lakini tukiendelea kusoma hatuitamki (Alif) tunasoma ‘Dhaqa-shshajarah’ ( فَلَمَّا ذَاقَا ٱلشَّجَرَةَ ).
4. Ikiwa imehadhifiwa (kuondolewa) nasi pia tuiondoe (hatuitamki) mfano: ( يَٰٓأَيُّهَ ) na **(يأْت)** Imeandikwa Alif kwenye (Ya Ayuha) nas tukisoma, tusome bila ya kuivuta. Mfano ( يَٰٓأَيُّهَ ٱلسَّاحِرُ )
   na neno Ya’ti, imeondolewa **(ي)** mwisho kwa hivyo tuisome kama ilivyoandikwa: **(يَوْمَ يَأْتِ لاَ تَكَلَّمُ نَفْسٌ)**.
5. '<u>Ta</u>' yakuonyesha mwanamke inaitwa **تَاءُ التَّأْنِيْث** Tau - tta’nith.
   Ikiandikwa <u>ta</u> marbutta (iliyofunga) **(ة)** tukisimama tunasimama kwa (ha) **(ه)** k.m **(سكرة – ربوة)** فَلَا ٱقۡتَحَمَ ٱلۡعَقَبَةَ ١١ tunasoma neno la mwisho aqaba<u>h</u> (sio kwa ta), na ikiwa imeandikwa ta iliyo wazi **(ت)** tukiisimamia <u>ta</u> hiyo tunaitamka 'Ta' **(رحمت – نعمت – لعنت)**
   Rahmat – Naamat – Laanat. K.m. يُنَادُونَكَ مِن وَرَآءِ ٱلۡحُجُرَٰتِ
   Tukisimama Hujuraat<u>i</u>; inabidi tuondoe kasra na tusimame kwa sukun “HUJURAA<u>T</u>”.

## ALAMA ZA KUSIMAMA AU VITUO                                                    علامات الوقف

1. KITUO CHA LAZIMA                                                    علامة الوقف اللازم

Mim ndogo (م) haina mkia. Hiyo ni alama ya kuonyesha kusimama kwa lazima (yaani lazima usimame kwenye neno lenye mim ndogo juu yake). Kwa mfano:-

Lazima kusimama kwenye ۞ إِنَّمَا يَسْتَجِيبُ الَّذِينَ يَسْمَعُونَ ۘ وَالْمَوْتَىٰ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ sukun)

2. La (لا) ni alama inayokataza kabisa kusimama! Kwa mfano:-        لا: علامة الوقف الممنوع

الَّذِينَ تَتَوَفَّاهُمُ الْمَلَائِكَةُ طَيِّبِينَ ۙ يَقُولُونَ سَلَامٌ عَلَيْكُمُ ادْخُلُوا الْجَنَّةَ

Usisimame kabisa kwenye neno ‘tayyibina’.

3. Alama ya ‘Jim’ ndogo (ج)

ج: علامة الوقف الجائز جوازاً مستوي الطرفين

juu ya neno unaweza ama kusimama au kuendelea; yote yanafaa. Kwa mfano:- نَحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ نَبَأَهُمْ بِالْحَقِّ ۚ إِنَّهُمْ فِتْيَةٌ آمَنُوا بِرَبِّهِمْ

Unaweza kusimama kwenye bil’haq au ukaendelea kusoma.

4. Alama ya Silaa (صلى) inafaa kusimama, lakini bora kuendelea, kwa mfano:        صلى:علامة الوقف الجائز مع كون الوصل أَولى

وَإِنْ يَمْسَسْكَ اللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُ إِلَّا هُوَ ۖ وَإِنْ يَمْسَسْكَ بِخَيْرٍ فَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

5. Alama ya Qilaa (قلى) قلى: علامة الوقف الجائز مع كون الوقف أولى

Unaweza kusimama au kuendelea lakini bora kusimama. Kwa mfano:

قُلْ رَبِّي أَعْلَمُ بِعِدَّتِهِمْ مَا يَعْلَمُهُمْ إِلَّا قَلِيلٌ ۗ فَلَا تُمَارِ فِيهِمْ

6. Alama ya Taanuq (∴ ∴) ukisimama kwenye علامة تعانق الوقف: ∴ ∴ moja ya maudhui mbili haifai kusimama juu ya nyengine. Kwa mfano:

ذَٰلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ ۛ فِيهِ ۛ هُدًى لِلْمُتَّقِينَ

ukisimama kwenye (لاريب) husimami kwenye (فيه) au unasimama kwenye (لاريب فبه) yaani kwenye ‘فيه’ husimami kwenye (لاريب).

Tutataja alama nyengine za kusimama ambazo unaziona katika Misahafu mengine nazo ni:

(1) Alama ya (Tta) (ط) ni alama ya ط: علامةٌ للوقفِ المطلق kusimama umuman ambayo wameiwafiqi Maulamaa wengi nao ni msimamo mzuri na unaposimama ukiendelea kusoma unaanza kwa neno lililo baada yake moja kwa moja.

(2) Alama ya msimamo mzuri. ح: علامةٌ للوقف الحسن

(3) Alama iliyoruhusiwa ص: علامةٌ للوقفِ المرخص لضرورةٍ kusimama kwa dharura.

(4) Alama ya ق: علامةٌ للوقفِ الذي لم يقُلْ به أكثرُ العلماءِ kusimama ambayo hawaitaji Maulamaa wengi ni alama dhaifu kwa hivyo kuendelea ni bora.

(5) Msimamo mfupi tu, khafifu. س: للسكتة اللطيفةِ

(6) 'Qif' ni alama inayopendelewa قف: علامةٌ للوقف المستحب kusimama, lakini ukiendelea kusoma hakuna makosa.

(7) 'Za' ni alama inayojuzu ama kusimama au kuendelea ز: kusoma, lakini bora kuendelea.

(8) Alama ya kuonyesha mwisho ع: علامةٌ لانتهاءِ العشر sehemu moja kwa kumi (1/10). Watu wengine huita mwisho wa qara. Katika Misahafu ya Kufiyyi العدَد الكوفي Ziko na nyingi nyinginezo katika Misahafu ya Kizamani ambayo maelezo yake hutiwa mwisho wa Misahafu hiyo. Lakini sisi tushughulikie zile alama za Misahafu yetu ya Asim kutokana na Hafs.

## ALAMA NYENGINE NI HIZI

Kuwekwa sifuri (ziro) ya duara juu ya وَضع الصِّفر المستدير ( ۟ )

herufi inayoitwa kwa Kiarabu (حرف علة) inayoonyesha kuongezeka kwa herufi ile lakini haitamkwi ukiendelea kusoma au ukisimama. Kwa mfano: . قَالُوا۟ · يَتْلُوا۟ صُحُفًا · لَأَا۟ذْبَحَنَّهُۥٓ · وَثَمُودَا۟ فَمَآ أَبْقَىٰ

Na kuwekwa sifuri ndefu iliyosimama **ووضعْ الصِّفر المستطيل القائم** ( ۠ ) juu ya alif ambayo baada ya herufi mutaharika (yaani yenye fat'ha, au kasra au dhamma) inayoonyesha kuzidi kwake unapoendelea kusoma lakini siyo unaposimama k.m.:

أَنَا۠ خَيْرٌ مِّنْهُ . لَّٰكِنَّا۠ هُوَ ٱللَّهُ رَبِّى . وَتَظُنُّونَ بِٱللَّهِ ٱلظُّنُونَا۠ هُنَالِكَ . كَانَتْ قَوَارِيرَا۠ قَوَارِيرَا۟ مِن فِضَّةٍ

na huachwa kutiwa hiyo sifuri juu ya alif ambayo baada yake herufi yenye sukun, ijapo hukumu yake ni sawa na inapokuwa herufi iliyo baada yake yenye haraka (yaani fat'ha au kasra au dhamma) huachwa ukiendelea kusoma, na hubakia ukisimama bila ya kuwepo kwake unapoendelea kusoma.

Kwa mfano: **أَنَا ٱلنَّذِيرُ** (Haikutiwa kwenye alif ya nuni).

Huwekwa kichwa cha 'Kha' **وضع رأس خاء صغيرة (بدون نقطة)** ndogo ( ۡ ) (bila ya nukta) na kwamba imedhihirika ambapo ncha ya ulimi inaigonga sehemu yoyote ya kinywa (na kuleta sauti ya herufi hiyo, huwa imetiwa sukun) K.m.

مِّنْ خَيْرٍ . يَنْهَوْنَ عَنْهُ . قَدْ سَمِعَ . أَوَعَظْتَ .

Lakini pia huondolewa sukun hiyo kwenye herufi inapoingizwa (yaani Id'gham) herufi hiyo ya kwanza katika ya pili; Id'gham kamili pamoja na kukaza herufi ya pili kwa kutiwa shadda. K.m.

أُجِيبَت دَّعْوَتُكُمَا. يَلْهَث ذَّٰلِكَ . وَقَالَت طَّآئِفَةٌ . وَمَن يُكْرِههُّنَّ

na vile vile katika maneno ya Mwenyezi-Mungu Mtukufu ambayo inaonyesha pande zote inapodhihirika sukun na inapoachwa.

(( أَلَمْ نَخْلُقكُّم )).

Imeondolewa sukun imetiwa sukun

Pia huachwa tupu herufi pasina kutiwa sukun wala kukaza herufi ya pili yake kuonyesha Id'gham ya herufi ya kwanza katika ya pili lakini Id'gham hiyo ni pungufu (si kamili ambayo hutiwa shadda) k.m. مِن وَالٍ . فَرَّطتُمْ . بَسَطتَ

Na kutiwa Mim ndogo (yenye mkia) **وضعُ ميم صغيرة (م)**

Badala ya haraka ya pili katika Tanween au juu ya nuni iliyotiwa sukun badala ya sukun (yaani huondolewa sukun na kutiwa mim ndogo badala yake. Haraka ya fat'ha au dhamma au kasra pia katika Tanween au nuni kuwa mim. K.m.

عَلِيمٌۢ بِذَاتِ ٱلصُّدُورِ . جَزَآءًۢ بِمَا كَانُوا۟ . مُّنۢبَثًّا

Na kupangwa haraka (وتركيب الحركتين: (ضمتين أوفتحتين أوكسرتين) mbili (dhammatein au fat'hatein au kasratein) kama hivi: ـٍ ـً ـٌ k.m.

سَمِيعٌ عَلِيمٌ · وَلَا شَرَابًا إِلَّا · وَلِكُلِّ قَوْمٍ هَادٍ

Na mpango wa pili wa haraka mbili inapoonyesha Id'gham kamili pamoja na kukazwa herufi ya pili yake kama hivi: ـٍ ـً ـٌ kwa mfano:-

خُشُبٌ مُّسَنَّدَةٌ · غَفُورًا رَّحِيمًا · وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاعِمَةٌ

Na huonyesha Id'gham pungufu kama mpango wa pili lakini herufi zifuatazo hazikazwi, k.m.

وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ · رَحِيمٌ وَدُودٌ

Na inapokuwa 'Ikhfaa' (**الإخفاء**) k.m. شِهَابٌ ثَاقِبٌ · سِرَاعًا ذَٰلِكَ · بِأَيْدِي سَفَرَةٍ كِرَامٍ

Na herufi ndogo ndogo zinazotiwa **والحروف الصغيرة** katika Misahafu ambazo huonyesha herufi zilizoachwa katika Misahafu Al Othmania ambazo inapasa kuzitamka unapotaka kusoma Qur'an. K.m.

يَلْوُونَ أَلْسِنَتَهُم · إِنَّ وَلِـِّۧىَ اللَّهُ · إِۦلَٰفِهِمْ رِحْلَةَ الشِّتَاءِ · وَكَذَٰلِكَ نُـۨجِى الْمُؤْمِنِينَ

Ikiwa herufi ilioachwa inayo badili yake katika uandishi wa asili zinafanywa katika kutamkwa herufi zilizoengezwa wala si zile zilizowekwa badala yake k.m. ٱلصَّلَوٰةَ · ٱلرِّبَوٰاْ · ٱلتَّوْرَىٰةَ

Na vile vile وَٱللَّهُ يَقْبِضُ وَيَبْصُۜطُ · فِى ٱلْخَلْقِ بَصْۜطَةً

Lakini ikiwekwa sin (س) chini ya (ص) huitamka kwa (ص) ni mashhuri zaidi k.m. ٱلْمُصَۣيْطِرُونَ

Kutiwa alama hii **وضع هذه العلامة** ( ~ )

Juu ya herufi huonyesha kuwa lazima herufi hiyo ivutwe mvuto zaidi kuliko ule mvuto wa Madda ya asili ya tabii. Kwa mfano

الٓمٓ · ٱلطَّآمَّةُ · قُرُوٓءٍ · سِيٓءَ بِهِمْ · شُفَعَٰٓؤُاْ · تَأْوِيلَهُۥٓ إِلَّا ٱللَّهُ ·

لَا يَسْتَحْىِۦٓ أَن يَضْرِبَ · بِمَآ أُنزِلَ

Wala haitumiki alama ya Madda kuonyesha Alif iliyoondolewa baada ya Alif iliyoandikwa kwa mfano ( **آمنوا** ) kama inavyokosewa katika baadhi ya Misahafu bali huandikwa hivi:

kwa Hamza na Alif: **ءامنوا**

Na duara ambayo ndani yake **والدائرة المحلاة** التى في جوفها رقم imetiwa nambari, ni kuonyesha mwisho wa Aya na kuonyesha ni Aya ya ngapi katika Sura fulani; haifai kutiwa kabla ya Aya kabisa kwa hivyo hutoiona duara hio mwanzo wa Aya bali huonekana mwisho wake.

إِنَّآ أَعْطَيْنَٰكَ ٱلْكَوْثَرَ ﴿١﴾ فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَٱنْحَرْ ﴿٢﴾ إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ ٱلْأَبْتَرُ ﴿٣﴾

Na hutiwa alama hii **وتدل هذه العلامة** ( ۞ )

Kuonyesha mwanzo wa juzuu na ahzaab na nusu na robo.

Na huwekwa alama hiyo ifuatayo kuonyesha mahali pa kusujudu na utaona kunawekwa mstari juu ya neno linalopasa sijida

**ووضع هذه العلامة** ( ۩ ) بعد كلمة يدل على موضع السجدة نحو:

وَلِلَّهِ يَسْجُدُ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِي ٱلْأَرْضِ مِن دَآبَّةٍ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةُ وَهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ ﴿٤٩﴾
يَخَافُونَ رَبَّهُم مِّن فَوْقِهِمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ ۩ ﴿٥٠﴾

## DUA YA KUSUJUDIA UNAPOSOMA QUR'AN

## دُعاءُ سُجُود التِّلاوَةِ

**(١) (( سَجَدَ وَجْهِيَ لِلَّذِي خَلَقَهُ،**
**وَشَقَّ سَمْعَهُ وَبَصَرَهُ بِحَوْلِهِ وَقُوَّتِهِ،**
﴿ فَتَبَارَكَ ٱللَّهُ أَحْسَنُ ٱلْخَٰلِقِينَ ﴾ )) (١)

**(٢) (( اللَّهُمَّ اكْتُبْ لِي بِهَا عِنْدَكَ**
**أَجْراً، وَضَعْ عَنِّي بِهَا وِزْراً، وَاجْعَلْهَا**
**لِي عِنْدَكَ ذُخْراً، وَتَقَبَّلْهَا مِنِّي كَمَا**
**تَقَبَّلْتَهَا مِنْ عَبْدِكَ دَاوُدَ)) (٢)**

Na hutiwa alama hii: ( ◊ ) **ووضع النقطة التالية الوسط المُعيِّنة الشكل**

Chini ya Ra (ر) katika Qauli yaKe tukufu: بِسْمِ ٱللَّهِ مَجْرٜىٰهَا

Alama hii huonyesha kutoitamka Fat'ha sawa sawa unaipelekea kwenye kasra na unaipelekea Alif kwendea Ya kwa hivyo hatuitamki Maj'raha wala Majriha bali baina yao na tunaisema MAJREHA. Vile vile inawekwa mwisho wa Mim karibu kidogo na Nuni iliyotiwa shadda katika Qauli yaKe Tukufu مَا لَكَ لَا تَأْمَ۫نَّا عَلَىٰ يُوسُفَ Inaonyesha kuikutanisha midomo kama kwamba unaitamka kwa dhamma kuonyesha haraka iliyoondoshwa ni dhamma (bila ya kudhihirika hiyo athari katika matamshi).

Na kutiwa nukta ya duara ( • ) **ووضع نقطة مدوّرة مسدودة الوسط**

Iliyofungwa juu ya Hamza ya pili kuwepesisha kutamka baina ya Hamza na Alif:
Surat Fussilat Aya ya 44. Tunaisoma 'Aa'jamiyun' ( ءَا۬عْجَمِيٌّ )

وَلَوْ جَعَلْنَٰهُ قُرْءَانًا أَعْجَمِيًّا لَّقَالُوا۟ لَوْلَا فُصِّلَتْ ءَايَٰتُهُۥٓ ءَا۬عْجَمِىٌّ

DARSA YA ISHIRINI NA MOJA

## السكتات الخمس والالفات السبع

Kusita kufupi kwa kiasi cha haraka mbili bila ya kupumua ambako kumekusudiwa kuendelea kusoma. Mifano mitano ijayo unasita kwenye kisin kidogo (س) na kuendelea kusoma ila mfano wa tano inafaa kusimama na kupumua, na kusita bila ya kupumua ina kuingiza katika herufi inayofuata nayo ni (هـ); yaani Id'gham.

١- وَلَمْ يَجْعَل لَّهُۥ عِوَجَا ۜ ﴿١﴾ قَيِّمًا (الكهف - ١)

٢- مَنۢ بَعَثَنَا مِن مَّرْقَدِنَا ۜ هَٰذَا مَا وَعَدَ الرَّحْمَٰنُ (يس - ٥٢)

٣- وَقِيلَ مَنْ ۜ رَاقٍ ﴿٢٧﴾ (القيامة - ٢٧)

٤- كَلَّا ۖ بَلْ ۜ رَانَ عَلَىٰ قُلُوبِهِم مَّا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿١٤﴾ (المطففين - ١٤)

٥- مَا أَغْنَىٰ عَنِّي مَالِيَهْ ۜ ﴿٢٨﴾ هَلَكَ عَنِّي سُلْطَانِيَهْ ﴿٢٩﴾ (الحاقة - ٢٨)

Unasimama msimamo mfupi kwenye 'ha' ya neno ﴿ مَالِيَهْ ﴾ kwa njia mbili: (a) Kuidhihirisha 'ha' (Maliyah) pamoja na kusita kidogo bila ya kupumua na kuendelea. (b) Kuiingiza 'ha' katika (ha) ya neno la pili nalo ni: ﴿ هَلَكَ ﴾ (Hivyo tumefanya Id'gham).

Vile vile inapasa kuthibitisha 'ALIF' inayoangukia mwisho wa maneno yafuatayo katika maandishi na kusimama, na inapasa kuiacha kuitamka unapoendelea kusoma.

١- أَلَفُ (أَنَاْ) ضميرِ المتكلمِ أينما ورَد في القرآنِ الكريم.

٢- أَلَفُ (لكناْ) من قولِهِ تعالى: لَّٰكِنَّا۠ هُوَ اللَّهُ رَبِّي (الكهف- ٣٨)

٣- ألف (الظنوناْ) من قوله تعلى: وَتَظُنُّونَ بِاللَّهِ الظُّنُونَا ﴿١٠﴾ (الأحزاب- ١٠)

٤- ألف (الرسولاْ) من قوله تعلى: وَأَطَعْنَا الرَّسُولَا ﴿٦٦﴾ (الأحزاب- ٦٦)

٥- ألف (السَّبِيلَاْ) من قوله تعلى: فَأَضَلُّونَا السَّبِيلَا ﴿٦٧﴾ (الأحزاب- ٦٧)

٦- أَلف (قواريراْ) من قوله تعلى: كَانَتْ قَوَارِيرَاْ (الإنسان-١٥)

٧- أَلف (سَلاَسِلاْ) من قوله تعلى: إِنَّآ أَعْتَدْنَا لِلْكَٰفِرِينَ سَلَٰسِلَاْ
(الإنسان-٤)

Ama katika tamko la ﴿ سَلَٰسِلَاْ ﴾ lina njia mbili katika kusimama kwake (a) Kuthibitika alifu ya mwisho (b) Kuiacha pamoja na kusimama kwenye Lamu iliyotiwa sukun, kama hivi: (سَلاَسِلْ).

## MATANABAHISHO

Nawatanabahisha machache yafuatayo:-

1. Mlijifunza kabla kwamba Al Madd Al Aridh المد العارض للسكون lissukun inafaa kuifupisha na kutawassuttisha (yaani kati kwa kati) na kuifanya Madda refu kwa kuitia sukun herufi ya mwisho (yaani unaweza kuifanya haraka mbili; au nne; au sita).

   Na nakuzidishia ujuzi kuwa inafaa katika Madda hii kusimama kwa:

   (a) Kuileta sehemu ya haraka iliyoqadiriwa thuluthi yake kwenye dhamma na kasra tu. Na njia hii huitwa kwa Kiarabu

   أ– الرّوم

   Yaani tukisimama kwenye herufi yenye dhamma au kasra ni juu yetu kuvuta Madd-Al-Aridh haraka mbili tu tena tunaileta sehemu ya dhamma au kasra k.m. (( نستعينُ – الدينِ )).

   (b) Na vile vile kwa kuikutanisha midomo miwili baada ya kutia sukun herufi iliyo na dhamma kwa ukamilifu ambapo mwerevu huin'gamua, wala haihisi asiyetumia akili yake.

   Njia hii huitwa 'Al Ishmaam' ب– الاشمام

   (Tutazitumia kwa Kiarabu)

   Tukisimama kwenye herufi yenye dhamma kwa 'Al Ishmaam' kwa hivyo tunaivuta Madd Al Aridh haraka mbili, au nne au sita. Tena tunaitia sukun herufi ya mwisho na kuipeleka midomo yetu mbele kidogo, mifano: (( نستعينْ – عظيمْ ))

   Inatokea ikaangukia 'Al Ishmaam' katikati ya neno (kwa mujibu wa Riwaya ya Hafs hii tunayojifunza) katika Qauli yake Mtukufu: Nayo katika Surat Yusuf tu Aya ya11

   ﴿مالك لا تأمنّا﴾

   Inayoonyesha kukutana midomo kwenye Nuni yenye dhamma iliyoachwa rasmi na kuwa Mudghima (Id'gham) wakati wa kuitamka, na huwa hivyo baada ya kutia sukun Nuni kwa ukamilifu.

   (c) Huitamki 'Arrum' wala 'Al Ishmaam' katika '<u>Ha</u>' ya kike ـة) ((رحمة – نعمة)) kwa sababu hamna 'Rumi' ndani yake wala 'Ishmaam', ikiwa herufi unayosimamia ni 'Ha'. Amma ukisimamia 'Ta' iwazi husimamia kwa Arrumi na Ishmaam, k.m. ((بَقِيَّتُ اللهِ . كَلِمَتُ ربِّكَ)).

(d) Haraka ya Kasra ina Rumi bila ya Ishmaam. Haraka ya Dhamma ina Rumi na Ishmaam.

2. Ikitangulia Hamzat el Istifham kwenye jina mahali pa

(AL) ATTAARIF (ال) التعريف

katika maneno yajayo → ((ءالذكرين – ءاللَّه – ءالئن)) inajuzu kwa Qiraa zote njia mbili:-

(a) Mabadiliko (الإبدالُ) yaani unaibadilisha Hamzatel-Wasl na kuifanya Madda refu na kuwa harakaat sita, na inakuwa hukumu yake ya 'MADDA ALLAZIM AL-MUTHAQQAL AL KALIMY' katika maneno mawili ((ءَآلذَّكَرَيْنِ – ءَآللهُ)) na huwa ALLAZIM AL MUKHAFAF AL KALIMY katika neno (ءَآلْئٰنَ) na wengine huiita MADDAL FAR'Q.

(b) Wepesi (التَّسْهِيْلُ) nako ni kutamka Hamza ya pili ambayo ni Hamzatel-Wasl baina ya Hamza na Alif

(ءَآلذَّكَرَينِ – ءآلله – ءَآلئن)

Nazo zimo katika Mahali au Maudhuu haya:

قُلْ ءَآلذَّكَرَيْنِ حَرَّمَ أَمِ ٱلْأُنثَيَيْنِ الأنعام/١٤٣ –١٤٤

ءَآلْـَٔنَ وَقَدْ كُنتُم بِهِۦ تَسْتَعْجِلُونَ يونس/٥١

ءَآلْـَٔنَ وَقَدْ عَصَيْتَ قَبْلُ يونس/٩١

قُلْ ءَآللَّهُ أَذِنَ لَكُمْ يونس/٥٩

ءَآللَّهُ خَيْرٌ أَمَّا يُشْرِكُونَ النمل/٥٩

Siri ya kubakia Hamzatel-Wasl katika mfano wa maneno hayo yaliyoanziwa na Hamzat el Istifhaam ili pasitokee kubabaishika ikiwa pataondoshwa Hamza. Lau ikiondolewa patatokea mbabaiko wa Hamza iliyobakia; ikiwa Hamzat el Istifham au Hamzatel-Wasl.

(P. S. Hamzat el Istifham ni Hamza inayoulizia suali, k.m. mfano wa juu wa kwanza baada ya "قُلْ" inakuja Hamzat el Istifham "Aaa dhakarayni". Tafsiri:- "Jee madume mawili wameharimishwa (au majike wawili ?) n.k."

3. Neno ( ءَاْعْجَمِيٌّ ) katika Qauli yake Tukufu

وَلَوْ جَعَلْنَٰهُ قُرْءَانًا أَعْجَمِيًّا لَّقَالُوا۟ لَوْلَا فُصِّلَتْ ءَايَٰتُهُۥٓ ءَا۬عْجَمِىٌّ وَعَرَبِىٌّ (فصلت– ٤٤)

Amesoma 'Hafs' hivyo kwa kusahilisha Hamza ya pili baina ya Hamza na Alif, na alama ya wepesi huo katika Msahafu Mtakatifu imetiwa nukta kubwa juu ya Hamza ya pili.
Inahitajia kuona na kuipata kwenye vinywa vya Wasomaji Wazuri (yaani uangalie wasomaji mahodari wanaposoma)

4. Inaonyesha hukumu ya Id'gham (ث) katika (ذ) katika Qauli yake Tukufu: يَلْهَث ذَّٰلِكَ الأعراف / ١٧٦

Pia Id'gham ya (ب) katika (م) k.m. inayoitwa إدغام المتجانسين

يَٰبُنَىَّ ٱرْكَب مَّعَنَا وَلَا تَكُن مَّعَ ٱلْكَٰفِرِينَ هود/٤٢

5. Na hukumu ya kudhihirisha (ن) katika : Yaaasi<u>n</u> – Noooo<u>n</u>

يسٓ ۝١ وَٱلْقُرْءَانِ ٱلْحَكِيمِ يس/١

نٓ ۚ وَٱلْقَلَمِ وَمَا يَسْطُرُونَ القلم/١

6. Katika neno ((مالِيَهْ)) katika Qauli yake Tukufu:

﴿ مَآ أَغْنَىٰ عَنِّى مَالِيَهْ ۜ ۝ هَلَكَ عَنِّى سُلْطَٰنِيَهْ ﴾ الحاقة/٢٨– ٢٩

Inafaa kusimama kwenye neno hilo kwa sababu ni mwisho wa Aya, na inafaa kuingiza (Id'gham) katika 'Ha' – هـ ya neno la pili lililoifuata na kuwa إدغام متماثلين na vile vile inafaa kuidhihirisha (Na kudhihirika huko hakutimii ila kwa kusita kufupi bila ya kupumua).

7. Neno ((ءاتن ے)) katika Qauli yake Tukufu:

فَمَآ ءَاتَىٰنِۦَ ٱللَّهُ خَيْرٌ مِّمَّآ ءَاتَىٰكُم النمل/٣٦

Ambayo imeandikwa bila ya 'Ya' lakini katika Qiraa ya Hafs imethibitiwa 'Ya' kwa fat'ha katika kuendeleza kusoma na inaondolewa ukiisimamia.

8. Neno ((ضعف)) katika mahali pake patatu

ٱللَّهُ ٱلَّذِى خَلَقَكُم مِّن ضَعْفٍ ثُمَّ جَعَلَ مِنۢ بَعْدِ ضَعْفٍ قُوَّةً ثُمَّ جَعَلَ مِنۢ بَعْدِ قُوَّةٍ ضَعْفًا وَشَيْبَةً ۚ يَخْلُقُ مَا يَشَآءُ ۖ وَهُوَ ٱلْعَلِيمُ ٱلْقَدِيرُ الروم/٥٤

Linasomwa neno hili kwa kutiwa fat'ha (ضَـ) na kulitia dhamma (ضُـ) zote mbili ni sahihi zinasomwa katika Rasm ya Hafs kutokana njia ya الشَّطِبِيّة وَالطيبة pamoja (tutaeleza njia hizo baadae) lakini kutiwa fat'ha kumewekwa mbele katika kusoma.

9. Haifichiki kuwepo 'HA' katika neno (فيه) linavutwa Madda Silat Qaseera katika maudhuu moja tu katika Qur'ani Tukufu nayo:

يُضَٰعَفْ لَهُ ٱلْعَذَابُ يَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ وَيَخْلُدْ فِيهِۦ مُهَانًا     الفرقان/٦٩

Na kuwa 'Ha' katika neno ((يرضه)) halivutwi kwa ajili ya 'Alif' ilioachwa kabla yake ambayo ilikuwa yenye sukun, kwa sababu ya jawabu ya sharti. (Sharti mshukuru ndipo Mwenyezi-Mungu Ataridhishwa kwenu)     الزمر/٧     وَإِن تَشْكُرُوا۟ يَرْضَهُ لَكُمْ

10. Inatakikana kutanabahi kwamba 'Ha' katika ((عليهُ)) ni yenye haraka dhamma na vile vile 'Ha' katika ((أنسنِيهُ))

وَمَنْ أَوْفَىٰ بِمَا عَٰهَدَ عَلَيْهُ ٱللَّهَ فَسَيُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا     الفتح/١٠

وَمَآ أَنسَىٰنِيهُ إِلَّا ٱلشَّيْطَٰنُ أَنْ أَذْكُرَهُۥ     الكهف/٦٣

Kama inavyopasa kutanabahi kulisoma neno ((يَتَّقْهِ)) katika

وَمَن يُطِعِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ وَيَخْشَ ٱللَّهَ وَيَتَّقْهِ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْفَآئِزُونَ     النور/٥٢

Hapa tunatia sukun kwenye (قْـ) na tunatia kasra kwenye (ـهِ) tunatamka 'wayattaq'hi'.

11. Mwanzo Surat al Imraan, Qauli yake Tukufu:

Inavutwa Mim -     الٓمٓ ﴿١﴾ ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلْحَىُّ ٱلْقَيُّومُ ﴿٢﴾

Maddan Lazim Mukhafafan Harfiyan; haraka sita ukisimama. Ama ukiendelea kusoma na kuuganisha na Jina la Mwenyzi-Mungu Mtukufu, hutiwa Mim ya mwisho; haraka ya Fat'ha kwa sababu zimekutana herufi mbili zenye sukun na unasema:

((مِيْمَ اللهُ)) na inajuzu kwa Wasomaji wote kuvuta Madda refu ya haraka sita kwa mujibu wa Asli (ya Madda hii), na Madda fupi ya haraka mbili kama ilivyowekwa kuwa kwa Fat'ha Al-Aridh.

12.Maneno haya ((ائْذَنَ– أؤتُمِنَ– ائتِ– ائْتُونِي)) katika Aya zifuatazo: ﴿وَمِنْهُم مَّنْ يَقُولُ ائذَنْ لِي وَلاَ تَفْتِنِّي﴾ التوبة/٤٩. ﴿فَلْيُؤَدِّ الَّذِي اؤْتُمِنَ أَمَانَتَهُ﴾ البقرة/٢٨٣

Tukiyaanzia maneno hayo juu zinakutanika Hamza mbili yenye haraka na yenye sukun kwa hivyo inapasa kubadilisha Hamza ya pili na kuwa herufi yenye Madda kutokana na aina ya haraka ya Hamza ya mwanzo na zinakuwa:

((إيذن– أوتمن– إيت– إيتوني)) ..الخ

(Hamza ya pili (ئـ) inakuwa herufi ya Madda na kuvutiwa 'Ya' kwa sababu tunaitamka Hamzatel-Wasl kwa kasra 'Idhan' ايذن).

13.Inalazimika kudhihirisha kila herufi kutoka kwenye Makhraj yake na kuipa Sifa yake kwa ukamilifu, na hassa ikiwa imetiwa sukun, hivyo hakukuwepo Id'gham. Inapasa kutanabahi kudhihirisha Mim yenye sukun inapokuwa herufi iliyo baada yake ni 'Waw' au 'Fa' kama vile vile inavyopasa kudhihirisha (Dhdhad -ض) ikiwa baada yake ni herufi ya (Tta- ط) au (Ta - ت) k.m. ((اضْطُرَّ – أَفَضْتُمْ)) Kwa sababu hakuna Id'gham katika maneno hayo.

Nalitaja kabla njia ya الشاطبية na الطيبة. Hao ni watungaji mashairi.

Tukianzia الشاطبية ni mashairi kwa jina la:

(حرز الأماني ووجه التهاني)

katika kuelezea Qiraa Saba zilizo maarufu katika usomaji wa Qur'ani. Na yameitwa kwa jina la Ash'shattibiya kwa mujibu wa mshairi huyu ambaye anaitwa

(القاسم بن فيُّره الشاطبي الرعيني الضرير) (٥٣٨هـ– ٥٩٠– هـ)

Ama الطيبة ni mashairi ya (طيبة النشر في القراءات العشر) na mtungaji wake anaitwa

(محمد بن محمد بن محمد الجزري الدمشقي) (٧٥١هـ– ٨٣٣هـ)

Beti zake zilizidi elfu.

MWISHO

# التكبير وختم القرآن

Inapendelewa kupiga Takbir kuanzia Sura ya ‘Adhuha’ au mwisho wake (hiyo Sura) mpaka mwanzo wa Sura ya ‘Annas’ au mwisho wake. Na imeendelea na kubakia kupiga Takbir kwa sababu ni maqamu ya Kutukuza na kuadhimisha kwa kuonea raha na ladha katika Kumtaja Mwenyezi-Mungu Mtukufu unapokhitimisha Kitabu Kitukufu.

Kutamka kwake ni (اللهُ أَكبرُ) na imesimuliwa kuongeza Tahlil nako ni kusema (لا إِلَه إِلا الله) na Tahmeed nako ni kusema (ولله الحمدُ) Na huanzwa hivyo kabla ya kusema: (بسم الله).

Inasuniwa ukikhitimisha Qur’ani (yaani ukimaliza Msahafu) na ukafika سورةِ النّاس (ambayo Sura ya mwisho) uendeleze kusoma kwa kuanzia Sura ya الفاتحة na kuanza kwa Sura البقرة mpaka (المفلحونَ) ili pawepo muungano wa usomaji na kudumu Kheri yake.

Inapendelewa pia baada ya kumaliza kukhitimisha Msahafu, kujishughulisha na dua zilizotajwa zinazoeleza kwamba Rehema Inashuka unapomaliza Msahafu. Imesimuliwa kwamba Mtume S.A.W. Amesema: Mwenye kusoma Qur’ani anakubaliwa Dua yake Mola Akitaka Humjibu kwa haraka katika dunia au Humwekea maombi yake Akhera.

Alikuwa Sahaba wa Mtume S.A.W. anayeitwa Anas bin Malik, Radhi za Mungu juu yake, akimaliza Msahafu hukusanya watu wake na kuomba dua na mwenye kuamini kukubaliwa dua yake.

Katika Dua iliyotokana na Mtume (S.A.W) ukimaliza kusoma Msahafu Mtukufu ni hii:

((اللَّهُمَّ ارْحَمْنِي بِالقُرآنِ ، واجْعَلْهُ لي إِمَاماً وهُدىً ونوراً ورحمةً ، اللَّهُمَّ ذكّرني منهُ ما نسيتُ ، وعلّمني منهُ ما جهلتُ ، وارزُقني تلاوَتهُ آناءَ اللَّيلِ وأَطرافَ النهارِ ، واجعلهُ لي حُجَّةً يا ربَّ العالمينَ.))

Na katika Dua iliyosimuliwa kutokana na Mtume (S.A.W) kupata Kheri za dunia na Akhera ni:

((اللَّهُمَّ إنا عبيدُك ، وأَبناءُ عبيدِك ، وأَبناءُ إِمائكَ ، ناصيتُنا بيدِكَ ، ماضٍ فينا حُكمُك ، عدلٌ فينا قضاؤكَ ، نسْأَلُكَ بِكُلِّ اسْمٍ هُو لكَ ، سمَّيْتَ بِهِ نفْسكَ ، أَوْ أَنْزلْتَهُ فِي كِتابِكَ ، أَوْ علَّمْتَهُ أَحدًا مِنْ خلْقِكَ ، أَوْ اسْتأْثَرْت بِهِ فِي عِلْمِ الْغيْبِ عِندكَ : أَن تجْعلَ الْقُرْآنَ الْعظِيمَ ربِيع قُلوبنَا ونُورَ أَبصارِنَا ، وشفاءَ صدورنا وجلاءَ أَحزانِنا ، وذهابَ همومِنا وغمومِنا وسائقَنا وقائدَنا إِليكَ وإِلى جنّاتِكَ ، جنّاتِ النّعيم ، ودارِكَ دارِ السّلامِ مع الّذين أَنعمتَ عليهم من النبيّين والصّدّيقين والشهداءِ والصالحينَ برحمتكَ يا أَرحمَ الرّاحمينَ)).

Na unamaliza Dua zako kwa:-

( سُبْحَٰنَ رَبِّكَ رَبِّ ٱلْعِزَّةِ عَمَّا يَصِفُونَ * وَسَلَٰمٌ عَلَى ٱلْمُرْسَلِينَ * وَٱلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ ).